Mothers' UNION

# Shajara ya Maombi 2021

Kuunganisha wanachama kwa sala na ibada kote duniani

Inajulikana kirasmi kama *Families Worldwide*

3-4 Barua la Raisi wa duniani kote

5 Utangulizi wa Shajara ya Maombi

6 Tafakari ya kipindi cha robo mwaka: Kuunganishwa kwa Maombi

7 Matokeo ya kazi yetu: Vikundi vya Vicoba vya Ushirika wa Akina Mama

20 Tafakari ya kipindi cha robo mwaka: Nguvu ya Maombi

33 Matokeo ya kazi yetu: Kupambana na “njaa ya likizoni” mjini Down & Dromore, Irelandi Kaskazini

34-35 Ramani ya wanachama

36 Matokeo ya kazi yetu: Mabadiliko ya jamii kupitia kujifundisha kilimo, kusoma na kuandika

38 Tafakari ya kipindi cha robo mwaka: Kudumu katika Maombi

52 Tafakari ya kipindi cha robo mwaka: Furaha ya Maombi

53 Matokeo ya kazi yetu: Mashine za kushona kwa wanawake wasiojiweza nchini Rwanda











## Shajara ya Maombi 2021


7 Januari
12 Februari
16 Machi
21 Aprilli
25 Mei
30 Juni
39 Julai
44 Agosti
48 Septemba
54 Oktoba
59 Novemba
63 Desemba


*The Prayer Diary* (Shajara ya Maombi) ni rasilimali ya kuongeza maarifa kwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, inayochapishwa mara moja kwa mwaka na kusambazwa kama sehemu ya usajili wa kila mwaka, kwa wanachama na marafiki walio Uingereza na Irelandi. Wanachama wa nchi za kigeni na marafiki wanaweza kupokea nakala ya PDF kupitia barua-pepe kutoka mikoa ya ndani au kwenye mtandao www.mothersunion.org. *The Prayer Diary* imetafsiriwa kwa lugha za Kifaransa, Kihispania cha Amerika Kusini na Kiswahili

Kwa mawasiliano
Mothers’ Union, Mary Sumner House,
24 Tufton Street, London, SW1P 3RB
T: 020 7222 5533
E: publications@mothersunion.org

www.mothersunion.org

**Namba ya usujili:** 240531

**Rais wa duniani kote:** Sheran Harper
**Mkurugenzi mkuu:** Bev Jullien

*The Prayer Diary* imechapwa na Mothers’ Union

**Mhariri:** Beth Lanksford
**Mbunifui:** Adam Austin
**Kimechapwa na:** Halcyon Print Management Ltd

Karatasi iliyotumika katika chapisho hili imetengenezwa kwa kutumia mbao kutoka misitu endelevu na isiyo na klorini.

Huku kila juhudi ikiwa imechukuliwa ili kuhakikisha usahihi wa tarehe na maoni, Ushirika wa Akina Mama hauwezi kukubali jukumu kwa hasara yoyote, uharibifu au usumbufu unaosababishwa kwa makosa yoyote au upungufu.

© hati miliki ya yaliyomo 2020

# *Marafiki wapendwa,,*

***Tulisikiliza! Hatua ndio hii!***

Kama kawaida, kila mwaka kuna jambo la kusisimua linalojitokeza katika maisha ya Ushirika wa Akina Mama. Hili ni jambo la kufurahisha kwani linatupa fursa mpya za kushiriki na kusherehekea pamoja kwa njia mbali mbali na za kutia moyo.

Kwa hivyo, 2021 sio tofauti wakati ninakuletea shajara yetu mpya ya maombi Prayer Diary ya kila mwaka inayohamasisha, ambayo inachukua kina cha maombi kutoka *Families Worldwide* na kuiunganisha na mipango mipya; kama tafakari ya ziada, na shuhuda za matokeo ya kazi yetu ulimwenguni.

Maombi ni muhimu kwa maisha na kazi yetu, na ninapendekeza *Prayer Diary* kuwa rafiki mwaminifu katika maisha yako kama mshiriki na katika kujitolea kwako kuinua wengine kwa maombi. Ukiiweka karibu nawe au kwenye kiti chako ukipendacho, itakusaidia kuwa na nia zaidi katika kutenga wakati wa kuomba kama familia ya kiulimwengu. Tena tutakuwa tukipata pamoja ufahamu na maombi mengi ambayo yataimarisha uhusiano wetu na Mungu na kila mmoja wetu, na kutia moyo imani yetu.

Nashukuru kila mshiriki na rafiki kwa upendo na msaada wako kwa ajili ya *Families Worldwide*; asante kwa wote ambao waliotuchangia kwa ukarimu ili kufanya chapisho hili liwe la kupendeza na sababu ya kusherehekea mabadiliko ambayo Ushirika wa Akina Mama unaleta; asante kwa wafanyikazi waaminifu ambao walifanya kazi kwa bidii ili yote yawezekane.

Mwaka 2020 umekuwa wa kunusurika na changamoto za janga la COVID-19, kutafuta njia mpya za kufanya kazi na kukabiliana, na kutambua kwamba Mungu wetu yu hai na bado anafanya miujiza. Ninaomba kwamba 2021 italeta mwanzo mpya, upya na uamsho kwa kila moyo, nyumba, jamii na taifa. Mwaka wa 2021 ukawe mwaka wa mafanikio huku tukiwa pamoja tunajenga tena matumaini na ujasiri katika kila nyanja ya maisha yetu na katika Ushirika wetu wa Akina Mama.

Kwa upendo wangu na baraka za Mungu kila wakati

*Sheran*

# Sura mpya ya duka la Ushirika wa Akina Mama katika mtandao

## Uchaguzi mpana wa bidhaa zenye alama ya Ushirika wa Akina Mama, beji, machapisho na zaidi. Tunawasilisha kote duniani

www.mueshop.org



# Sala ya Ushirikiano

### Jiunge na wanachama wenzako wa Ushirika wa Akina Mama kote ulimwenguni tunaposaidia familia na miradi kote ulimwenguni kwa njia ya maombi

Maombi yapo katikati ya kazi yetu kama Ushirika wa Akina Mama na kila siku, saa sita mchana, washiriki ulimwenguni kote husimama na kufanya maombi. Wimbi la Maombi ni dhihirisho endelevu la kujitolea kwa kuombeana kati yetu, maombi ambayo yanaendelea mwaka mzima na yanajumuisha maeneo yote ambayo tunawakilishwa.


Unaweza kutumia maombi haya ya kila siku kujiunga na Wimbi hili la Maombi kila siku masaa 24 kote ulimwenguni, ukiombea majimbo kwa zamu. Kalenda imegawanywa katika sehemu za siku tatu wakati tunaombea kikundi cha dayosisi. Siku moja ya juma kuna aya ya Biblia ambayo unaweza kutafakari juu yake na kuchukua fursa ya kuombea vipengele vya kazi ya Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote ambavyo umevutiwa navyo wakati huo.

Tunapochukua jukumu letu katika kudumisha Wimbi la Maombi, tunaweza kufanya hivyo kwa kujiamini, tukijua sala zetu zina maana na nguvu. Tunaweza kutiwa moyo pia kwa kujua kwamba ulimwenguni kote kuna wengine ambao, kwa njia ile ile, wanatuombea. Na sasa kwa kuwa Shajara ya Maombi ya kila mwaka inatafsiriwa kwa Kifaransa, Kihispania na Kiswahili ni rahisi zaidi kwetu kuombeana.

> Tunamshukuru Mungu daima kwa ajili yenu nyinyi nyote na kuwakumbukeni daima katika sala zetu
>
> **1 Wathesalonike 1:2**

Yesu, Bwana wa uzima, kwa nguvu ya neno lako na kupitia matendo yako ya upendo, tuite tuwe wanafunzi wako. Tupe nguvu ya kuwa tofauti, kusimama kwa haki na amani na kuwa ishara za upendo wako wa kupatanisha watu wote.
Mungu wa neema, wawezeshe watumishi wako kutekeleza utume wako duniani kupitia kazi ya Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni. Leo tunaombea
** tazama shajara ya Wimbi la Maombi.*

Tunawaombea washiriki wote. Mungu awe pamoja nao katika kila sehemu ya maisha yao, awatie moyo na kuwaongoza, awahifadhi na kuwapa nguvu ili waweze kufanya kazi kwa sifa na utukufu wako. Amina



# Kuungana katika sala



## Januari-Machi

**Imeandikwa na Thembsie Mchunu, Mdhamini wa Ukanda wa E**

**Maandiko matakatifu:** **Kwa maana popote pale wanapokusanyika wawili au watatu kwa jina langu, mimi nipo hapo kati yao.** *(Mathayo 18:19-20)*

Watu wengi kutoka Msumbiji, Zimbabwe na nchi nyingine jirani wameweza kusaidia familia zao kwa ajili ya kazi ambayo walikuwa wakifanya nchini Afrika Kusini. Tangu COVID-19, maeneo mengi ya kazi yamefungwa na wafanyikazi hao hawaruhusiwi kuja Afrika Kusini kutafuta kazi nyingine.

Hata ndani ya nchi, tunakabiliwa na kiwango cha juu cha uhalifu, pamoja na wizi, utekaji nyara wa magari, na wizi wa kuvunja nyumba n.k. Vijana wanatafuta njia za kupata mali haraka. Nyumbani kuna mivutano mingi ya kifedha au mali ambayo husababisha unyanyasaji wa kijinsia, vipigo na ubakaji. Maisha ni magumu kweli katika ukanda wetu. Jamii katika Sudan na Sudan Kusini pia zinakabiliwa na umaskini, jambo ambalo linamaanisha kuwa unyanyasaji wa majumbani unaongezeka.

Baba wa Mbinguni, tunasifu jina lako na tunakuabudu kwani wewe bado ni Mungu hata katika nyakati mbaya. Ulitufundisha kwamba 'mwili umeunganishwa ingawa umeundwa na sehemu nyingi. Kwa hiyo ikiwa sehemu moja inateseka, kila sehemu inateseka pia. (1 Wakorintho 12:12 na 26) Kama



wanachama wa Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote, tunaungana katika maombi na ahadi yako kwamba 'ambapo wawili au watatu wanakusanyika kwa jina lako, hapo utakuwa pamoja nao.' Tafadhali ponya kila mwanadamu na udhihirishe kuwa kila mmoja wetu ameumbwa kwa mfano wako. Bwana kwa rehema yako, sikia maombi yetu!

## Wazo la maombi

- Ulimwengu mzima uko kwenye machafuko kutokana na COVID-19. Eneo letu linakabiliwa na kiwango cha juu cha ukosefu wa ajira kwani sehemu nyingi za kazi zimefungwa. Tafadhali omba ili kazi zifunguliwe kwa usalama.
- Kwa ajili ya wale wanaokabiliwa na ukatili wa kijinsia na unyanyasaji wa majumbani.
- Ili uhalifu upunguke katika ukanda wetu na ulimwenguni kote.

# Matokeo ya kazi yetu

## Matokeo ya kazi yetu: Vikundi vya MU Vicoba




Vicoba ni mpango wetu wa Mikopo na Akiba nchini Tanzania. Tuna washiriki zaidi ya 5,000 katika vikundi 218. Kutoka kwa akiba ambayo vikundi vimekusanya na mikopo ambayo wanapata kutoka kwa kila mmoja, vikundi vyote vya MU Vicoba vinaripoti kuwa wanachama wanatumia mikopo yao sana sana kuanzisha biashara ndogondogo ambazo zinanufaisha familia zao. Kwa mfano, Daisy ni mwanachama wa kikundi cha MU Vicoba huko Dayosisi ya Masasi. Alitumia mkopo kuanzisha biashara ya usagaji wa unga. Kutokana na faida ya biashara yake ya unga, aliweza kuanzisha mikondo miwili zaidi ya mapato - kutengeneza na kuuza sabuni na mafuta ya nazi. Kwa kipato cha Daisy kilichoongezeka, anaweza kuwapatia watoto wake wawili chakula bora, kuwalipia ada ya shule na kuwanunulia vifaa vya shule.

Mwanachama mwingine wa MU Vicoba, Helen, kutoka Kanisa Kuu la Anglikana huko Zanzibar, alichukua mkopo kutoka kwa kikundi chake na akautumia kuchimba kisima cha kina kifupi nyumbani kwake, ili kuwezesha familia yake kupata maji safi, na wakati huo huo akaanzisha biashara mbili ndogo - kunenepesha mifugo na kunyunyuzia mazao ya mboga ya mzunguko mfupi ambayo yeye huuza sokoni. Helen na kikundi chake cha MU Vicoba wametumia mapato haya ya ziada katika biashara zao kupata bima ya kitaifa ya afya kwa kila mwanakikundi na familia zao.

# Furahi na Tafakari

## Januari 1-2 2021

### Ijumaa 1

Ikiwa huu utakuwa Mwaka Mpya wa Furaha, mwaka wa manufaa, mwaka ambao tutaishi kuifanya dunia hii kuwa bora zaidi, ni kwa sababu Mungu ataongoza njia yetu. Ni muhimu sana basi, kuhisi utegemezi wetu kwake! *Matthew Simpson, 1811-1884*

### Jumamosi 2

Bwana wa Upendo, tunapochukua hatua za kwanza kwenye njia ya mwaka huu mpya, tunafurahi kwa ukweli kwamba utakuwa rafiki yetu wa kila wakati katika heka heka za yote yaliyoko mbele. Tunafurahi kwa ahadi yako ya kwamba kamwe hutatuacha au kututelekeza.

### Wimbi la Maombi

**Januari 1-3:** Wadhamini wote wa Ushirika wa Akina Mama na wafanyakazi kote duniani

# Maono ya siku zijazo Januari 3-9 2021

### Jumapili 3
Bwana, matukio ya jana yamepita na hatuwezi kuyabadilisha. Tupe ujasiri na maono tunapoingia katika siku zijazo, tukiamini kuwa utakuwa taa yetu ituongozayo na kutulinda katika safari yetu.

### Jumatatu 4
Jisifieni jina lake takatifu; wenye kumcha Mwenyezi-Mungu na wafurahi. Mwendeeni Mwenyezi-Mungu mwenye nguvu; mwendeeni Mwenyezi-Mungu daima. *1 Nyakati 16: 10-11*

### Jumanne 5
Bwana, tunapotafuta kujenga tena tumaini na ujasiri katika maisha ya watu kufuatia janga la ulimwengu, tunaomba utupe maono yako ya siku njema zaidi zijazo.

### Jumatano 6 Epifania
Wajuzi walisafiri umbali mrefu kumtafuta mtoto Yesu. Tunapomtafuta pia, nasi pia tusafiri kwenda kwenye mioyo na akili zetu na tutampata. Yeye yuko pamoja nasi siku zote.

### Alhamisi 7
Bwana, utupe maono dhahiri ya mustakabali wa Ushirika wa Akina Mama ili tuzidishe rasilimali zetu na kufanya kazi pamoja kwa ufanisi. Tuhamasishe na maoni na ubariki mipango yetu ili tufikie lengo letu la ulimwengu ambapo upendo wa Mungu unaonyeshwa kupitia uhusiano wa upendo, heshima na kustawi.

### Ijumaa 8
Asante Bwana kwa kutupa imani kwako. Tunaweka maisha yetu ya baadaye mikononi mwako tunapofuata kule ambako unatuelekeza. Tuhamasishe na maono yako na ututie nguvu ya Roho wako.

### Jumamosi 9
Mungu wa wakati na nafasi, inua macho yetu kupita wakati wa sasa. Furika macho ya mioyo yetu kwa nuru na kupanua maono yetu ya milele. Kaza macho yetu kwa Yesu, aliyevumilia msalaba, kwa ajili ya furaha iliyowekwa mbele yake: utukufu wa milele katika mkono wa kulia wa Mungu.

### Wimbi la Maombi

**Januari 1-3:** Wadhamini wote wa Ushirika wa Akina Mama na wafanyakazi kote ulimwenguni

**Januari 5-7:** Swaziland; Ruaha, Tanzania; Aguata na Lagos Mainland, Nijeria; Norwich, Uingereza na Chotanagpur, India

**Januari 8-10:** Lesotho; Kibungo, Rwanda; Etche & Ogbomoso, Nijeria; Leeds, Uingereza na Hanuato, Visiwa vya Solomon

# Ushirika wa Akina Mama Duniani kote

## Januari 10-16 2021

### Jumapili 10
Leo tunasherehekea kwa furaha familia ya Ushirika wa Akina Mama; tunaunganisha mikono kwa ushirika na washiriki wetu kote ulimwenguni. Na tuungane pamoja kwa kusudi tunapotafuta kujenga tena tumaini na ujasiri kwa wale tunaowahudumia.

---

### Jumatatu 11
Mtang'ara kati yao kama nyota zinavyoliangaza anga,  mkishika imara ujumbe wa uhai. *Wafilipi 2: 15-16 (BHN)*

---

### Jumanne 12
Baba wa Mbinguni, tunawaombea wamiliki wa ofisi ya Ushirika wa Akina Mama kote ulimwenguni. Wape utambuzi na neema ya kukumbuka mahitaji ya wale ambao wameitwa kuwatumikia.

---

### Jumatano 13
Ushirika wa Akina Mama uendelee kukua pamoja katika imani, matumaini na upendo, na kuleta baraka hizi ulimwenguni. *Rachel Carnegie: Muungano wa Anglikana.*

---

### Alhamisi 14
Bwana, tunakushukuru kwamba sisi kama Ushirika wa Akina Mama tunashikana mikono kote ulimwenguni kusaidiana. Tunawaombea leo wanachama wetu ambao wanakabiliana na hali ngumu sana maishani mwao.

---

### Ijumaa 15
Mungu mwenye Neema, tunakusifu kwa maisha na mahusiano mengi ambayo yamebadilishwa na uchungaji wa washiriki wetu ulimwenguni kote. Tunaomba utoaji wako wa rasilimali unaoendelea ili tuweze kuendelea kuwa ushawishi wa ulimwengu kwa kutenda mema.

---

### Jumamosi 16
Chukua muda leo kuwaombea washiriki wa  muungano wa dayosisi yako au kwa ajili ya mipango inayotekelezwa kote ulimwenguni ambayo inakuvutia na unayoyajali.

### Wimbi la Maombi

**Januari 8-10:** Lesotho; Kibungo, Rwanda; Etche & Ogbomoso, Nijeria; Leeds, Uingereza na Hanuato, Visiwa vya Solomon

**Januari 12-14:** Mauritius; Kericho, Kenya; Katsina,Nijeria; Kumasi, Ghana; Winchester, Uingereza na Nandyal, India

**Januari 15-17:** Shelisheli; Bukedi, Uganda; Enugu, Nijeria;  Birmingham, Uingereza na Marathwada, India

# Undugu wa Kikristo Januari 17-23 2021

## Jumapili 17
Bwana, tusaidie sisi sote kutembea katika nuru kama wewe ulivyo nuruni. Utusogeze pamoja kwa upendo, tuunganishe katika ushirika, na utuimarishe na kumtia nguvu kila mmoja wetu katika mwendo wetu wa Kikristo.

## Jumatatu 18
Kwa sasa, ndugu …. Muwe na ukamilifu, shikeni mashauri yangu, muwe na nia moja; kaeni kwa amani. Naye Mungu wa upendo na amani atakuwa pamoja nanyi.
*1 Wakorintho 13:11 (BHN)*

## Jumanne 19
Omba kwa ajili ya vikundi vya Kikristo vya madhehebu tofauti ili washiriki pamoja, kwa furaha mpya na ushirika, na kujitolea kufanya zaidi pamoja.

## Jumatano 20
Baba Mungu, tusaidie kuombea matunda ya ukaribu wa ushirika wa Kikristo, tukipendana kama vile ulivyotupenda, ili tuweze kusherehekea kukaa katika upendo wako kupitia umoja kati yetu na mshikamano mkubwa zaidi pamoja na uumbaji wote.

## Alhamisi 21
Bwana, tunakuomba utulete pamoja tuwe kitu kimoja katika maombi na sifa; kila siku tuinuane kwenye kiti chako cha neema.

## Ijumaa 22
Mungu mwenye rehema, linda na ujalie kila mshiriki wa Kanisa lako duniani kote na utoe msaada wako, faraja na nguvu kwa wote ambao wanakabiliwa na majaribu, taabu na mateso ambayo yanapatikana katika ulimwengu wetu wa leo.

## Jumamosi 23
Bwana wa Upendo, asante kwa ushirika wa Wakristo tunaofurahia. Umetufanya tuwe kitu kimoja, kila mmoja na karama na talanta zake.

### Wimbi la Maombi

**Januari 15-17:** Shelisheli; Bukedi, Uganda; Enugu, Nijeria; Birmingham, Uingereza na Marathwada, India

**Januari 19-21:** St Mark the Evangelist, Afrika Kusini; Butare, Rwanda; Okigwe-Kusini, Nijeria; Gambia; British Columbia, Canada na Rajasthan, India

**Januari 22-24:** Misri; Gasabo, Rwanda; Otukpo & Pwani, Nijeria; Bathurst, Australia na Nasik, India

## Jumapili 24

Yesu alisema, “Heri walio masikini wa moyo, kwa maana watamwona Mungu”. Tunawaombea wale ambao ni ‘maskini moyoni’, ambao wanahisi hawapendwi na hawahitajiwi; tuwatambue, tuwathamini na tuwaonyeshe upendo wako ili waweze kukua kwa kujiamini na kuja kukukubali katika maisha yao.

## Jumatatu 25

Anayemsaidia maskini anamkopesha Mwenyezi-Mungu; Mwenyezi-Mungu atamlipa kwa tendo lake jema. *Methali 19:17*

## Jumanne 26

Yesu alisema, “Heri walio maskini wa roho maana ufalme wa mbinguni ni wao”. Tusaidie Bwana kuwatia moyo wale ambao wanahisi wamepotea na hawana matumaini.

## Jumatano 27

Tunakumbuka wale wote waliopoteza riziki zao katika janga la mwaka jana, wakati wanajenga tena maisha yao. Tunaomba wapate njia mpya za kutumia talanta na ustadi wao kujazwa na kupata pesa za kutosha kuwaendeleza wao na familia zao.

## Alhamisi 28

Omba leo kwa ajili ya shule zilizo katika maeneo maskini zaidi ulimwenguni, ambazo hazitoi elimu tu, bali chakula, mavazi, na huduma ya matibabu.

## Ijumaa 29

Leo tunafikiria wale ambao ni maskini katika maeneo tajiri ya ulimwengu wetu, ambapo watu wana aibu kukubali mahitaji yao. Tunawaombea warudishiwe hadhi yao na wapate msaada wanaohitaji ili waishi kwa raha na kujiamini siku hadi siku

## Jumamosi 30

Tunawaombea wote wanaoishi katika hali duni na usumbufu, kwa sababu hawana njia ya kupata pesa kununua chakula na mavazi. Tunatoa shukrani kwa wale wanaofanya kazi katika maeneo haya ili kuwapa tumaini na ujuzi wa kuboresha maisha yao.

### Wimbi la Maombi

**Januari 22-24:** Misri; Gasabo, Rwanda; Otukpo & On the Coast, Nijeria; Bathurst, Australia na Nasik, India

**Januari 26-28:** False Bay, Afrika Kusini; Shinyanga, Tanzania; Umuahia & Ijebu Kusini Magharibi, Nijeria; Bath & Wells, Uingereza na Vellore, India

**Januari 29-31:** Masvingo, Zimbabwe; Kibondo, Tanzania; Nebbi, Uganda; Bida, Nijeria; Llandaff, Wales na Kanyakumari, India

### Jumapili Januari 31

Leo unapokuja kuabudu, fungua moyo wako ili nuru ya Yesu iangaze katika pembe zenye giza kabisa za ulimwengu wako ; nuru ya Yesu ikuondolee kiza cha kukata tamaa na kukujaza matumaini na amani.

---

## FEBRUARI

### Jumatatu 1

Nimeuona wokovu wako ambao umewaandalia watu wote. Yeye ni nuru ya kufunua; Mungu kwa mataifa, naye ndiye utukufu wa watu wako Israeli. *Luka 2: 3- 32 (BHN)*

---

### Jumanne 2

Nuru ya Yesu na ionyeshwe katika kazi ya Ushirika wa Akina Mama ndani na ulimwenguni. Tuwe na msukumo na maono yake kwa sehemu yoyote ya ulimwengu ambayo tumeitwa kuhudumu na tuweze kujulikana kama watoaji nuru katika maeneo yenye kivuli.

---

### Jumatano 3

Bwana wa Upendo, tunatoa shukrani kwa kuwa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama wanaangaza kama vinara, na kuleta tumaini na ujalishi kwa wale tunaowahudumia.

---

### Alhamisi 4

Bwana Mungu maneno na matendo yetu yaonyeshe nuru ya upendo wako katika jina la Yesu. Tunapotembea maishani, ututie moyo ili tuangaze nuru yako kwa njia bora zaidi, ambayo inaweza kufikia wale walio na hitaji kubwa zaidi.

---

### Ijumaa 5

Baba wa Mbinguni tunajua kwamba Yesu yuko pamoja nasi akiangaza njia zetu wakati wa shida na uchungu na tunatoa shukrani kwa kutujali kwake kila wakati, hasa pale njia iliyo mbele ikionekana ina giza.

---

### Jumamosi 6

Tunakushukuru, Bwana, kwamba, kwa neema yako, sisi ni nuru ya ulimwengu. Na tuangaze zaidi nuru ya upendo wako tunapoishi imani yetu kwa vitendo.

### Wimbi la Maombi

**Januari 29-31:** Masvingo, Zimbabwe; Kibondo, Tanzania; Nebbi, Uganda; Bida, Nijeria; Llandaff, Wales na Kanyakumari, India

**Februari 2-4:** Matlosane, Afrika Kusini; Mumias , Kenya; Eha-Amufu, Nijeria; Ballarat Australia; Niagara, Canada na North Kerala, India

**Februari 5-7:** Botswana; Marsabit, Kenya; Idah & Jebba, Nijeria; Salisbury, Uingereza na Andaman & Car Visiwa vya Nicobar, India

## Jumapili 7
Tunafurahi katika uhusiano wetu kama wanachama wa Umoja wa Akina Mama ulimwenguni kote.

## Jumatatu 8
Muwe na moyo mwema na wenye kuhurumiana mpole [wenye huruma, wenye kuelewana]; kila mmoja na amsamehe mwenzake [kwa urahisi na kwa uhuru] kama naye Mungu alivyowasamehe nyinyi kwa njia ya Kristo. *Waefeso 4:32 (BHN)*

## Jumanne 9
Bwana, asante kwa mfano mzuri wa uhusiano ambao tunauona katika Utatu. Nguvu za Roho wako Mtakatifu zitutie nguvu katika uhusiano wetu wote, na upendo wako usiojua mwisho.

## Jumatano 10
Familia nazifanye kazi pamoja kuunda uhusiano thabiti kulingana na maneno ya Yesu 'Pendaneni kama vile mimi nimewapenda ninyi'.

## Alhamisi 11
Baba, tunakushukuru kwa watu wote ambao umetuzingira nao. Tudumishe tukiwa wenye kupendana na kujaliana katika uhusiano wetu wote, ili tuweze kuishi pamoja kwa amani.

## Ijumaa 12
Tufundishe Bwana kuwa wenye kuelewana na wavumilivu kwa kila mmoja wetu, kutambua kwamba tofauti zinaweza kuzaa matunda na kwamba tunaweza kujifunza kutoka kwa kila mmoja wetu.

## Jumamosi 13
Makosa mengi katika ndoa, malezi, huduma, na mahusiano mengine ni kutofaulu kusawazisha neema na ukweli. Wakati mwingine tunapuuza mambo yote haya mawili. Mara nyingi tunachagua moja juu ya jingine. *Randy Alcorn, mwandishi wa Amerika.*

### Wimbi la Maombi

**Februari 5-7:** Botswana; Marsabit, Kenya; Idah & Jebba, Nijeria; Salisbury, Uingereza na Andaman & Car Visiwa vya Nicobar, India

**Februar i9-11:** Lainya, Sudan Kusini; Ankole, Uganda; Abuja & Lagos-Magharibi, Nigeria; Lichfield, Uingereza na Karnataka Kaskazini, India

**Februari 12-14:** Matana, Burundi; Ankole Kusini, Uganda; Morogoro, Tanzania; Ohaji / Egbema, Nijeria

# Tafakari juu ya Kwaresima Februari 14-20 2021

### Jumapili 14
Baba Mungu, tunapojiandaa kuadhimisha Msimu wa Kwaresima, tusaidie kufanya maamuzi ya busara juu ya jinsi tunavyopaswa kufanya hivi.

### Jumatatu 15
Mioyo yetu yamtumainia Mwenyezi-Mungu. Yeye ni msaada wetu na ngao yetu. Naam twafurahi kwa sababu yake; tuna matumaini katika jina lake takatifu. Fadhili zako zikae nasi, ee Mwenyezi-Mungu, kwani sisi tumekuwekea tumaini letu. *Zaburi 33: 20-22*

### Jumanne 16
Tunatazamia kwa hamu kipindi cha Kwaresima na fursa za sala ya kina zaidi na masomo yalioimarika. Na tuchukue fursa hizi kujifunza, kukua na kukuza imani yetu na kujitolea kwetu.

### Jumatano 17 Jumatano ya Majivu
Bwana Yesu, tunapokumbuka wakati wako wa kufunga na kuomba jangwani, tusaidie kuwa na nguvu katika azimio letu la kukuiga katika ibada zetu.

### Alhamisi 18
Bwana, ulikabiliwa na changamoto kubwa pindi ulipokuwa kule jangwani. Kuwa na wale ambao maisha yao yameathiriwa na umasikini na makazi duni. Wabariki wote wanaofanya kazi kupunguza uzito wa hali zao na utuonyeshe jinsi sisi pia, tunaweza kuwasaidia ili maisha yao yawe rahisi.

### Ijumaa 19
Bwana, tuko mwanzoni tu mwa msimu huu wa Kwaresima. Tupe uvumilivu na dhamira katika maadhimisho yetu ili, kama wewe, “tusizimie wala kushindwa”.

### Jumamosi 20
Kwaresima kati yetu inachochea kuliruhusu Neno la Mungu lipenye maishani mwetu na kwa njia hii tujue ukweli wa kimsingi: sisi ni akina nani, tunatoka wapi, ni wapi tunapaswa kwenda, ni njia gani tunapaswa kuchukua maishani. *Papa Benedict XVI*

### Wimbi la Maombi

**Februari 2-14:** Matana, Burundi; Ankole Kusini, Uganda; Morogoro, Tanzania; Ohaji / Egbema, Nijeria; New Westminster, Canada na Dornakal, India

**Februari 16-18:** Bentiu, Sudan Kusini; Bunyoro Kitara , Uganda; Okigwe-Kaskazini na Omu-Aran, Nijeria; Kilmore, Elphin & Ardagh, All Ireland na Krishna-Godavari, India

**Februari19-21:** Free State , Afrika Kusini; Bondo, Kenya; Ogbia & Offa , Nijeria; Swansea & Brecon, Wales na Argentina

# Mambo ya Biashara yenye Haki Februari 21-27 2021

## Jumapili 21

Bwana mwenye huruma, tufundishe kuelewa, kutia moyo na kuhamasisha tunapotafuta kutenda kama mikono na miguu yako, katika jukumu letu la kutunza familia yetu ya ulimwengu kote duniani.

## Jumatatu 22

Shamba la maskini hutoa mazao mengi,lakini bila haki hunyakuliwa. *Methali 13:23*

## Jumanne 23

Leo tunawakumbuka wakulima wanaokuza mazao na mafundi kwenye warsha za jamii. Wape hekima na busara katika kufanya maamuzi.

## Jumatano 24

Tunaomba kwamba upendo na haki ya Mungu itabadilisha sheria na utendaji wa biashara. Tunaombea utendewaji wa usawa kwa wote wanaohusika katika mfumo wa biashara yenye haki.

## Alhamisi 25

Bwana naomba tuhimize maduka ya rejareja na maduka makubwa ya eneo letu kutoa ahadi halisi kuhusu biashara ya haki. Tunapofanya chaguo letu natuweze kuimarisha uhusiano wetu kupitia kukua kwa uelewa kwetu kuhusu miundo isiyo ya haki.

## Ijumaa 26

Bwana wa matumaini, utupe maono na nguvu ya kusema na kutetea biashara ya usawa, haki na upendo. Tutie moyo tuchukue jukumu letu katika kuwakomboa watu ulimwenguni kote ambao wamenaswa na umaskini uliokithiri.

## Jumamosi 27

Mwenyezi Mungu, tunawaombea hekima na dhamiri thabiti ya kijamii wale walio katika nafasi za madaraka, ili waweze kufanya maamuzi chanya na makubwa kufikia maisha ya masikini ulimwenguni.

## Wimbi la Maombi

**Februari 19-21:** Free State, Afrika Kusini; Bondo, Kenya; Ogbia & Offa, Nijeria; Swansea & Brecon, Wales na Argentina

**Februari 23-25:** Wau, Sudan Kusini; Kigeme, Rwanda; Bauchi, Nijeria; St David, Wales na Mandalay, Myanmar

**Februari 26-28:** Mundri, Sudani Kusini; Madi & Nile Magharibi, Uganda; Isikwuatu, Nijeria

# Wanawake wa Ushawishi Februari 28 - Machi 6 2021

## Jumapili 28

Tunamshukuru Mungu kwa Mary Sumner ambaye kupitia ushawishi wake ameufanya Ushirika wa Akina Mama kuwa namna ulivyo leo. Tunawaombea akina mama na wale wanaolea watoto, ili kwa maombi yao, upendo, vitendo na utunzaji waweze kuwafundisha na kuwaongoza watoto katika njia wanayopaswa kwenda.

## MACHI

## Jumatatu 1

Mwanamke amchaye Mwenyezi-Mungu atasifiwa. Jasho lake lastahili kulipwa, Shughuli zake hazina budi kuheshimiwa popote. *Methali 31: 30-31*

## Jumanne 2

"Ni nani ajuaye pengine umefanywa malkia kwa ajili ya wakati kama huu!?' *Esta 4:14* Waombee wanawake wanaopaza sauti dhidi ya dhuluma wanayoiona karibu nao.

## Jumatano 3

Tukumbuke wanawake katika uwanja wa umma walio na nafasi za mamlaka: wanasiasa, wale wanaofanya kazi katika vyombo vya habari, kanisani, katika biashara na katika elimu. Mungu awape hekima ya kutimiza jukumu lao lenye ushawishi kwa faida ya wote.

## Alhamisi 4

Tumshukuru Mungu kwa wanawake wengi ulimwenguni leo ambao wanajitahidi kuwa na athari nzuri kwa wengine kupitia maombi yao ya utulivu na thabiti.

## Ijumaa 5 Siku ya Maombi ya Wanawake Duniani

Leo tunaomba haswa kwa ajili ya wanawake wa Vanuatu, pamoja na wanachama wa Ushirika wa Akina Mama, kwani wamehamasisha Siku ya Maombi Duniani mwaka huu..

## Jumamosi 6

Leo tujiombee sisi wenyewe kama watu wenye ushawishi juu ya wale tunaowasiliana nao. Mungu wetu mwaminifu naatusaidie kuwatia moyo wengine kupitia yote tunayofanya kwa jina lake.

### Wimbi la Maombi

**Februari 26-28** Mundri, Sudan Kusini; Madi & Nile Magharibi, Uganda; Isikwuatu, Nijeria; Chichester, Uingereza na Seoul, Korea Kusini

**Machi 2-4:** Yei, Sudan Kusini; Luweero, Uganda; On the Lake, Nijeria; Grafton, Australia; Armagh, All Ireland na Kerala Kusini, India

**Machi 5-7:** Bujumbura, Burundi; Maseno Kusini, Kenya; Ihiala, Nijeria; Kamerun; Calgary, Canada na Ysabel, Visiwa vya Solomon

### Jumapili 7
Bwana mwenye upendo, fungua mioyo yetu Bwana ili tuweze kukujua vizuri zaidi, ili kwamba tunapokua katika imani, tutambue kuwa uko karibu nasi katika kila hali.

### Jumatatu 8
Hapo mtaweza kuishi kama anavyotaka Bwana na kutenda daima yanayompendeza. Maisha yenu yatakuwa yenye matunda ya kila namna ya matendo mema na mtazidi kukua katika kumjua Mungu. *Wakolosai 1:10*

### Jumanne 9
Baba, tusaidie kukua ili tuwe kama wewe kwa njia ya maombi, kusoma Biblia na kutamani uwepo wako, katika maisha yetu yote.

### Jumatano 10
Mungu mwenye Neema, tupe hekima ya kukutambua na kukuelewa wewe na sisi wenyewe kupitia neema ya Roho wako Mtakatifu ambaye ni Roho wa kweli.

### Alhamisi 11
Bwana mwenye haki, tusaidie kukua katika imani, ili kila tunachofanya kwa jina la haki, ukweli na wema, tujue kwamba tunafanya kwa jina lako.

### Ijumaa 12
Bwana, tunaomba kwamba wakati wa shida na taabu, tuweze kupata ukuaji mkubwa zaidi wa kiroho, badala ya kuteleza kurudi nyuma na kuachana na upendo wako.

### Jumamosi 13
‘Mtu yeyote anaweza kuwa Mkristo wa zamani. Kiujumia kinachotakikana ni muda. Sio kila mtu anakuwa Mkristo mkomavu.’ Bwana, tusaidie kukua katika ukomavu wa kiroho na vile vile katika idadi ya miaka ambayo tumekufuata.

### Wimbi la Maombi

**Machi 5-7:** Bujumbura, Burundi; Maseno Kusini, Kenya; Ihiala , Nijeria; Kamerun; Calgary, Canada na Ysabel, Visiwa vya Solomon

**Machi 9-11:** Awerialj, Sudan Kusini; Mityana, Uganda; Uyo & Ajayi Crowther, Nijeria; Rupert’s Land Canada na Patna, India

**Machi 12-14:** Port Elizabeth, Afrika Kusini; West Ankole , Uganda; Nomadic Mission & Ekiti-Kwara, Nijeria; Worcester, Uingereza na Episcopal Church of the Philippines

## Jumapili 14 Jumapili ya Mama Mlezi

Mungu mwenye upole, katika siku hii tunakuletea sala zetu za shukrani kwa ajili ya akina mama wote. Wape ujasiri ambao Maria alikuwa nao wakati wanawatunza na kuwathamini wale wote walio chini ya uangalizi wao.

## Jumatatu 15

Hivi ndivyo asema Bwana: Kama vile Mama anamfariji mtoto wake ndivyo nitakavyokufariji. *Isaya 66:13*

## Jumanne 16

Tunashukuru kwamba kupitia kazi ya Ushirika wa Akina Mama tuna uwezo wa kulea na kuwatunza wale walio na mahitaji katika ulimwengu wako wote, tunaposhiriki upendo wa Mungu kwa njia za vitendo.

## Jumatano 17

Leo tunawakumbuka katika sala zetu wale wote ambao mama zao hawako nao tena. Nawaijue faraja ya Kristo na kujali kwake kwenye huruma wanapowakumbuka mama zao milele ndani ya mioyo yao.

## Alhamisi 18

Tunatoa shukrani zetu za dhati kwa wale wanaofanya kazi katika huduma za utunzaji kama walezi, wafanyakazi wa kijamii na majukumu mengine muhimu, kwani wanatoa upendo wao na msaada wa kila wakati kwa watoto walio katika mazingira magumu katika jamii zetu.

## Ijumaa 19

Bwana wa upendo, tunashukuru milele kwa mafanikio ya mpango wetu wa ulezi wa Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote.

## Jumamosi 20

Bwana Yesu tunawaombea akina mama na walezi wote ambao wanahangaika wanapowahudumia watoto wa kila rika. Tafadhali watie moyo na uwaimarishe, na uwalete pamoja nao wale ambao wanaweza kuwasaidia mzigo na kutoa msaada wa vitendo.

### Wimbi la Maombi

**Machi 12-14:** Port Elizabeth, Afrika Kusini; West Ankole, Uganda; Nomadic Mission & Ekiti-Kwara, Nijeria; Worcester, Uingereza na Kanisa la Maaskofu la Ufilipino

**Machi 16-18:** Kajo-Keji, Sudan Kusini; Tarime, Tanzania; Dutse & Akoko-Edo, Nijeria na Canterbury, Uingereza

**Machi 19-21:** Antisiranana, Madagaska; Busoga, Uganda; Yola & Oke-Ogun, Nijeria; Algoma, Canada na Jabalpur, India

# Mambo ya Kimataifa

Machi 21-27 2021

## Jumapili 21

Bwana wa upendo, vunja kuta ambazo zinagawanya na uwaongoze wale wanaotafuta amani kati ya mataifa. Na watu wote waheshimu haki na mila za wengine na watumainie hekima na upendo wako.

## Jumatatu ya 22

Bwana Mwenye Enzi Kuu ataonyesha haki yake kwa mataifa ya ulimwengu. Kila mtu atamsifu! *Isaya 61:11 (NLT)*

## Jumanne 23

Tunaomba ili mahusiano mazuri yajengwe kwa kuzingatia uelewano zaidi, huruma na mawasiliano ya wajibu.

## Jumatano 24

Bwana tunawaombea viongozi wa ulimwengu wanaohusika katika majadiliano magumu ya kimataifa ili wasikilizane wao wenyewe na pia wale wanaowawakilisha.

## Alhamisi 25 Siku ya Mabibi

Baba wa Mbinguni ulimchagua Maria kuwa Mama wa Bwana wetu Yesu Kristo; tusaidie kufuata mfano wake wa utiifu na uaminifu tunapojibu kwa upendo wale wanaotafuta msaada wetu na kukuza ukuaji wa maisha ya Kikristo katika ulimwengu wako.

## Ijumaa 26

Tunauombea Umoja wa Mataifa unaoshughulikia maswala ambayo yanavuka mipaka na kuathiri ulimwengu wote. Maendeleo ya kweli nayafanyike juu ya kugeuza mjadala kuwa vitendo, huku wakitambua kila mara haki sawa na utu wa watu wote.

## Jumamosi 27

Bwana, kama washiriki wa shirika hili la kimataifa tuweze kuendelea kuchukua jukumu letu katika kuhudumia jamii tunamoishi, na kuonyesha upendo kwa majirani zetu katika sehemu zote ulimwenguni.

### Wimbi la Maombi

**Machi 19-21:** Antisiranana, Madagaska; Busoga, Uganda; Yola & Oke-Ogun, Nijeria; Algoma, Canada na Jabalpur, India

**Machi23-25:** Rokon, Sudani Kusini; Kampala, Uganda; Kaduna, Nijeria; Koforidua, Ghana; Brisbane, Australia na Peru

**Machi 26-28:** Zambia ya Kati, Zambia; Southern Highlands, Tanzania; Ogbaru & Badagry, Nijeria; Bermuda na Chandigarh, India

# Nguvu ya Maombi



## Aprili-Juni

**Imeandikwa na Kathleen Snow, Mdhamini wa Ushirika wa Akina Mama wa Kanda B**

**Maandiko matakatifu:** Sala ya mtu mwema ina nguvu ya kutenda mengi.. *(Yakobo 5:16)*

Baraka moja wakati wa janga la COVID-19 ni jinsi wanachama wetu wa Ushirika wa Akina Mama walivyokusanyika pamoja ulimwenguni kwa njia ya maombi. Tuliombeana kupitia WhatsApp, Zoom, wakati wa Maombi ya Mchana kwenye Facebook na ikiwezekana, tulionana ana kwa ana, huku tukijitenga kimwili na kuvaa barakoa. Tulifanya kile tunachofanya vizuri - wakati tunakabiliwa na majaribu, tunasali.



Maombi yetu huleta mabadiliko - Mungu hatuangushi kamwe. Anajibu maombi yetu kwa wakati wake na kwa njia yake. Yeye husikia maombi yetu tunapovuta maisha yetu pamoja. Lakini tunaweza kuvurugwa kutomlenga Yesu wakati maisha yetu yapo kwenye machafuko. Petro alivurugwa wakati Yesu alimwalika atembee juu ya maji ili akutane naye. Tunahitaji kuweka mwelekeo wetu kwa Yesu na kulia 'msaada!' tunapozama.

Jon, kuhani na rafiki alishiriki nami, 'Yote ni juu ya Yesu. Yesu ni mkubwa na anatusimamia na hajatoka kwenye jengo hili '. Alinikumbusha mambo matatu ambayo tunaweza kufanya:

1. Omba mwongozo.
2. Subiri mwelekeo.
3. Fuata mwelekeo.

Na umwachie Yesu yote!

## Hoja za maombi

- Kwa hekima na mwongozo kwa watu wa Brazil na USA, na kwa viongozi wao kutoa mwelekeo mzuri katika kuzuia na kushinda ugonjwa huu.
- Kwa nguvu endelevu ya wanachama wa Ushirika wa Akina Mama katika West Indies na Amerika Kusini wakati wanajitahidi kudumisha afya njema na uhusiano mzuri katika nyumba zao na jamii.
- Kwa amani, upatanisho na umoja huko USA wakati wanapambana na mgawanyiko na ubaguzi kati ya watu wao.

# Wiki Takatifu Machi 28 – Aprili 3 2021

**Jumapili 28** Jumapili ya Mtende
Wengi waliompokea Yesu kwa kelele za "Hosana" hawakudumisha furaha yao, kwani waliathiriwa na wale ambao hawakutambua upendo wa Mungu. Kama sehemu ya umati huo, na tumpokee Yesu maishani mwetu na tusipotoshwe na wengine.

**Jumatatu 29**
Mwana wa Mtu hakuja kutumikiwa, bali kutumikia, na kutoa maisha yake kuwa fidia ya watu wengi [kuwalipia bei ili wawe huru na adhabu ya dhambi]. *Mathayo 20:28 (BHN)*

**Jumanne 30**
Bwana Mpendwa, tunakupa yote tuliyo nayo, yote tunayofanya, yote tunayosema, na yote tunayofikiria; tunakabidhi maisha yetu kwako, ili tupate kuwa kama wewe, siku hadi siku.

**Jumatano 31**
Wakati Kwaresma inakaribia kumalizika, tunafikiria juu ya wanafunzi ambao walikwenda kuandaa Chumba cha Juu kwa ajili ya chakula chako cha mwisho hapa duniani. Natujitayarishe kupokea wokovu wako, na kukumbuka amri yako ya "kupendana sisi kwa sisi".

**APRILI**
**Alhamisi 1** Alhamisi Kuu
Siku hii tunapokumbuka ushirika wa kwanza, naomba tushiriki mkate uliovunjwa na divai iliyomwagwa kuwa kitu kimoja nawe na wote wanaoshiriki chakula hiki.

**Ijumaa 2** Ijumaa Kuu
Siku hii adhimu ulilipa bei ya mwisho kwetu. Natuangalie maisha yetu na tukiri dhambi zetu, ili Siku ya Pasaka tufurahi katika msamaha.

**Jumamosi 3**
Yesu, tunapokukumbuka ukiwa umekufa kaburini, tunawaombea wote wanaokata tamaa, ili wafufuke kutoka gizani na kuingia katika mwanga wa maisha.

## Wimbi la Maombi

**Machi 26-28:** Zambia ya Kati, Zambia; Southern Highlands,Tanzania; Ogbaru & Badagry, Nijeria; Bermuda na Chandigarh, India

**Machi 30 –Aprili 1:** Toamasina, Madagaska; Mukono, Uganda; Ikwerre & Ife Mashariki, Nijeria; Down & Dromore, All Ireland na Delhi, India

**April 2-4:** Umzimvubu, South Africa; Lweru, Tanzania; On the Niger, Nijeria; Cape Coast, Ghana; Ontario, Canada na Limerick & Killaloe, All-Ireland

# Utukufu wa ufufuo

Aprili 4-10 2021

## Jumapili 4 Jumapili ya Pasaka

Aleluya, Kristo amefufuka! Amefufuka kweli kweli, Aleluya! Tunakusifu kwa ushindi wako juu ya dhambi na tunafurahi kwa ufufuo wako mtukufu.

## Jumatatu 5

Kama Kristo alivyofufuliwa kutoka kwa wafu kwa utukufu wa Baba, sisi pia tunaweza kutembea katika maisha mapya. *Warumi 6: 4*

## Jumanne 6

Bwana uliyefufuka, baada ya kufufuka kwako ulikuja kwa wanafunzi wako kupitia milango iliyofungwa. Milango ya mioyo yetu naiwe wazi kila wakati kwako ili tuweze kujua mwongozo wako na ushirika wetu tunapoendelea na hija yetu ya Kikristo.

## Jumatano 7

Bwana uliyefufuka, maneno yako ya kwanza kwa wanafunzi wako yalikuwa "Amani iwe nanyi". Na tuijue amani yako katika maisha yetu leo na kila siku, na tuwe waleta amani popote tunapokuwa na ushawishi.

## Alhamisi 8

Tuwe na huruma kwa wote waliojeruhiwa kimwili, kiakili au kiroho na kuwa kituo cha upendo wako tunapowafikia kwa huruma na kukubalika.

## Ijumaa 9

Tusaidie kujua uwepo wa upendo wako ambao unatuongoza, kututia moyo na kutuimarisha wakati wote.

## Jumamosi 10

Nuru, mbingu, mashamba na bahari husifu Mungu anayepanda juu ya nyota, akiwa amezivunja sheria za kuzimu. Tazama, Yeye aliyesulubiwa anatawala kama Mungu juu ya vitu vyote, na vitu vyote vilivyoumbwa vinatoa maombi kwa Muumba wao. *Venantius, Kuhani wa Karne ya 6 na Mshairi*

### Wimbi la Maombi

**Aprili 2-4:** Umzimvubu, Afrika Kusini; Lweru, Tanzania; On the Niger, Nijeria; Cape Coast, Ghana; Ontario, Canada na Limerick & Killaloe, All Ireland

**Aprili 6-8:** Cueibet, Sudani Kusini; Gahini, Rwanda; Wusasa & Ibadan, Nijeria na Christchurch, New Zealand

**Aprili 9:** Nord Kivu, DR Congo; Kigali, Rwanda; Kiteto & Kubwa, Nijeria; Perth Australia na Kuranagala, Sri Lanka

# Kuwa na kiasi



### Jumapili 11
Kuwa na kiasi hakumanishi kupungukiwa. Kuwa na kiasi ni juu ya kuthamini zaidi vitu ambavyo ni muhimu. *Mwandishi hajulikani.* Bwana, tusaidie leo kuthamini vitu rahisi vya maisha na kuchukua muda kutafakari juu ya yale ambayo ni muhimu kwetu.

### Jumatatu 12
Sijishughulishi na mambo makubwa au masomo magumu sana kwangu. Badala yake, nimeridhika na nina amani. Kama mtoto analala kimya mikononi mwa mama yake, ndivyo moyo wangu ulivyotulia ndani yangu. *Zaburi 131: 1-2*

### Jumanne 13
Bwana unayetupenda, tusaidie kushukuru kwa kile tunacho na kukumbuka kuwa furaha hupatikana katika kuwa na kiasi, badala ya kusumbuka tukitafuta raha zisizoeleweka na za kuvutia sana ambazo hupatikana katika maisha ya karne ya 21.

### Jumatano 14
Baba wa Mbinguni, hauhitaji tulete sala ndefu zilizochanganuliwa ili tufurahishe. Kwa hiyo leo tunakuomba kwa njia sahili, utulize dhoruba katika maisha yetu.

### Alhamisi 15
Tusaidie kuonyesha sifa hizi katika kazi zote tunazofanya katika Ushirika wa Akina Mama, na kuonyesha upendo wa Yesu kwa matendo yetu sahili ya fadhili.

### Ijumaa 16
Tunaomba leo kwa imani nyepesi, kama ya mtoto kwa ajili ya washiriki wetu ulimwenguni kote ili wapate kujua amani na faraja ya upendo wa Mungu wetu maishani mwao na kujazwa na furaha inayotokana na kumfuata Kristo.

### Jumamosi 17
Yesu anatupa ujumbe huu rahisi lakini wenye kina ‘Usijali kuhusu kesho; kesho itajitunza. ‘ *Mathayo 6: 25-34.*

### Wimbi la Maombi

**Aprili 9-11:** Nord Kivu, DR Kongo; Kigali, Rwanda; Kiteto & Kubwa, Nijeria; Perth, Australia na Kuranagala, Sri Lanka

**Aprili 13-15:** Yirol, Sudani Kusini; Ruvuma, Tanzania; Nike & Benin, Nigeria; Canberra & Goulburn, Australia na Dogura, Papua New Guinea

**Aprili 16-18:** Kindu, DR Kongo; Mlima Kenya Magharibi, Kenya; Egbu, Nigeria; Te Pihopatanga O Aotearoa, New Zealand; Cork, Cloyne & Ross, Ireland yote na Himalaya za Mashariki, India

## Jumapili 18

Bwana mwenye upendo, tunawaombea wale wanaotembea pamoja nasi wakishiriki katika kazi, wakishiriki kwa maono na kusonga mbele kujenga Ufalme wako hapa duniani. Utupe masikio ya kusikiliza, macho yanayofunguka na midomo ambayo inazungumza juu ya upendo wako, tumaini, uzuri, amani, na rehema.

## Jumatatu 19

Bwana amekuambia yaliyo mema, na hii ndio anayohitaji kwako: kufanya yaliyo sawa, kupenda rehema, na kutembea kwa unyenyekevu na Mungu wako. *Mika 6: 8*

## Jumanne 20

Kristo mwenye upendo, utusamehe tamaa zetu za ubinafsi, ututie moyo katika safari yetu ya kiroho na utuwezeshe kutembea katika njia zako kila wakati, huku tukitamani kukutumikia kwa upendo na utumishi.

## Jumatano 21

Bwana, katika safari yetu na wewe, tuongoze kupingana na miundo isiyo ya haki na kutembea kwa amani na upatanisho ndani ya mioyo yetu.

## Alhamisi 22

Bwana Yesu, umetutafuta na unatujua. Unatuita kutoka kwa usalama wa mashua zetu kutembea na imani juu ya maji kuelekea kwako. Hata tunapojikwaa na kuanguka unatufikia ili kutuokoa na kututuliza.

## Ijumaa 23

Bwana wa maisha, kutembea nawe kunazalisha fadhili, huruma, haki na unyenyekevu - hii inaweza kuwa kielelezo cha maisha yetu ya kila siku. Na tuwe macho kwa hazina za kiroho na mafunzo ya maisha safarini na tuwe tayari kushiriki haya na wale ambao tunakutana nao.

## Jumamosi 24

Bwana, kuwa kiongozi wetu: kule utakapotuongoza tutafuata, pale ambapo utasimama tutangojea, tukisafiri pamoja kama mahujaji wa Kristo.

### Wimbi la Maombi

**Aprili 16-18:** Kindu, DR Kongo; Mlima Kenya Magharibi, Kenya; Egbu, Nijeria; Te Pihopatanga O Aotearoa, New Zealand; Cork, Cloyne & Ross, Ireland yote na Himalaya ya Mashariki, India

**Aprili 20-22:** Kinshasa, DR Kongo; Victoria Nyanza, Tanzania; Ahoada & Warri, Nijeria; Oxford, Uingereza na Port Moresby, Papua New Guinea

**Aprili 23-25:** Kisangani, DR Kongo; Kagera, Tanzania; Awka, Nijeria; Sunyani, Ghana; Manchester, Uingereza na Popondota, Papua New Guinea

# Hali ya kuwa tofauti

## Aprili 25 - Mei 1 2021

### Jumapili 25
Hebu tutoe shukrani leo kwa safari zetu tofauti za kiroho ambazo kila mmoja wetu anazofanya, ambazo zinatuleta pamoja katika sala na sifa tukisherehekea Baba yetu wa Mbinguni.

### Jumatatu 26
Mungu ameweka sehemu katika mwili, kila moja, kama vile alivyotaka iwe. Ikiwa zote zingekuwa sehemu moja, mwili ungekuwa wapi? Kama ilivyo, kuna viungo vingi, lakini mwili mmoja. *1 Wakorintho 12: 18-20*

### Jumanne 27
Chukua muda wa kusikiliza, kuona, kugusa na kuhisi hali ya kutatanisha na kutegemeana katika maumbile, na ulete maelewano kwa ulimwengu unaotuzunguka.

### Jumatano 28
Tunamsifu Mungu leo kwa vikundi vya watu ambao, kila mmoja ana ujuzi wake maalum, mafunzo na uzoefu tofauti, na wao hufanya kazi pamoja kuleta matumaini na uponyaji katika hali za dharura kote ulimwenguni.

### Alhamisi 29
Tunafurahi leo katika utofauti wa watu wanaoitikia wito wa Mungu. Bwana, katika tofauti zetu tuna lengo moja kuwa sehemu ya nuru yako tukufu, kwani tunapojiunganisha pamoja nuru inaangaza zaidi.

### Ijumaa 30
Hakujaonekana ulimwenguni maoni yoyote mawili yanayofanana, au nywele mbili au nafaka mbili; ubora wa ulimwengu wote ni utofauti. Bwana, tuongoze ili tusherehekee utofauti wa wanachama wa Ushirika wa Akina Mama tunapofikia jamii zetu tofauti.

### MEI
### Jumamosi 1
Chukua muda wa kutafakari juu ya tofauti ya miaka, tamaduni, lugha na vipaji vinavyopatikana katika familia ya kanisa lako, marafiki na jamii, na kutoa shukrani kwa utajiri unaoletwa kwenye maisha yako.

### Wimbi la Maombi

**Aprili 23-25:** Kisangani, DR Kongo; Kagera, Tanzania; Awka, Nijeria; Sunyani, Ghana; Manchester, Uingereza na Popondota, Papua New Guinea

**Aprili 27-29:** Port Sudan, Sudan; Muhabura, Uganda; Niger Delta Magharibi na Yewa, Nijeria; Wilaya ya Kaskazini, Australia na Chennai, India

**Aprili 30- Mei 2:** Aru, DR Kongo; Kigezi, Uganda; Ikeduru, Nijeria; Ho, Ghana; York, Uingereza na Guyana & Suriname, Guyana

# Biashara na viwanda

Mei 2-8 2021

## Jumapili 2

Leo tunatoa shukrani kwa biashara na viwanda ambavyo vitatimiza mahitaji yetu katika wiki ijayo. Tunatoa shukrani kwa ajira na bidhaa na huduma zinazotolewa na tunaombea afya na ustawi wa wote wanaofanya kazi katika biashara au viwandani.

## Jumatatu 3

Usimdhulumu jirani yako wala kumwibia. Mshahara wa mtu aliyeajiriwa usikae kwako usiku kucha hadi asubuhi. *Walawi 19:13 (GNT)*

## Jumanne 4

Tunawaombea wafanyabiashara walio peke yao, biashara ndogondogo na biashara mpya. Tunawaombea amani ya akili na utulivu kwao wote katika nyakati ngumu; tunaomba kuwe na uhusiano mwema kati ya biashara, na kati ya wote wanaofanya kazi pamoja katika biashara hizo.

## Jumatano 5

Tunawaombea wote wanaoajiri wengine, wawe na ustadi na hekima wanapofanya kazi pamoja, wapate rasilimali za kutunza wafanyakazi, wawe na mahusiano mazuri, na ya haki kati ya waajiri na waajiriwa.

## Alhamisi 6

Tunawaombea wote wanaofanya kazi katika tasnia ya huduma, wapate nguvu na hekima. Tunawaombea haswa kwa ajiili ya wale ambao wanahisi kuwa kazi yao inachukuliwa kuwa ya kawaida, au haithaminiwi.

## Ijumaa 7

Tunawaombea watengenezaji wa bidhaa na usalama kwa wale walio hatarini katika kazi yao viwandani vya utengenezaji wa bidhaa.

## Jumamosi 8

Tunaombea huduma za kifedha na wote wanaofanya kazi katika sekta hii. Tunaomba uadilifu katika shughuli zote za kifedha, na usambazaji wa usawa wa utajiri ulimwenguni kote, haswa wakati wa kutokuwa na uhakika wa kifedha.

### Wimbi la Maombi

**Aprili 30 – Mei 2:** Aru, DR Kongo; Kigezi, Uganda; Ikeduru, Nijeria; Ho, Ghana; York, Uingereza na Guyana & Suriname, Guyana

**Mei 4-6:** Uppershire, Malawi; Eneo la Wamishonari Maralali, Kenya; Makurdi & Ifo, Nijeria; Tuam, Killala & Achonry, Ireland yote na Mumbai, India

**Mei 7-9:** Torit, Sudan Kusini; Meru, Kenya; Ikwuano, Nijeria; Sekondi, Ghana na The Arctic, Canada

# Mtazamo wa Milele

Mei 9-15 2021

## Jumapili 9

Baba wa Mbinguni, asante kwa zawadi ya uzima wa milele, tuliyopewa kupitia upendo mkuu wa mwanao, Bwana wetu Yesu Kristo, ambaye kwa hiyari alijitoa mhanga kwa ajili yetu.

## Jumatatu 10

Taabu tunayopata ni kidogo, tena ya muda tu; lakini itatupatia utukufu upitao matazamio yote, utukufu ambao hauna mwisho. Hivyo tunatazamia kwa makini si vitu vinavyoonekana, bali visivyoonekana. Maana vinavyoonekana ni vya muda tu; lakini vile visivyoonekana ni vya milele. *2 Wakorintho 4: 17-18*

## Jumanne 11

Bwana, wewe ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, kwa hivyo tunakuomba utusaidie kuishi kwa mtazamo wa umilele, tukiamini kwamba utatuhimiza kufanya kile tunachohitaji kukamilisha na kwamba utakuwa pamoja nasi tutakapoenda kusikojulikana.

## Jumatano 12

Asante Bwana, kwamba ujuzi wa uzima wa milele unatusaidia kuishi siku hii tukijua kwamba chochote tunachokabiliana nacho leo tunaweza kushinda.

## Alhamisi 13 Siku ya Kupaa

Bwana uliyefufuka, tunaposherehekea kupaa kwako tunakuona wewe ukirudi kwa Baba yako mbinguni kukaa mkononi wa kulia wa Mungu katika utukufu. Tunakutolea siku hii ili tuiishi kwa njia inayopendeza machoni mwako.

## Ijumaa 14

Bwana Mpendwa, umenijua kwa nyakati zote na utanijua milele. Asante kwa kunipenda vile nilivyo na kuniandalia mahali huko mbinguni.

## Jumamosi 15

Bwana wa Milele, kiongozi wangu na rafiki yangu, ninakupa yote nilivyo. Nijulishe njia ulionitayarishia na ulenge moyo wangu na akili yangu juu ya mapenzi yako ili uweze kuniongoza kwa upole kwenye safari uliyopanga.

### Wimbi la Maombi

**Mei 7-9:** Torit, Sudani Kusini; Meru, Kenya; Ikwuano, Nijeria; Sekondi, Ghana na The Arctic, Canada

**Mei 11-13:** Twic Mashariki, Sudan Kusini; Rorya, Tanzania; Owerri na Ughelli, Nijeria; Gippsland, Australia na Cashel & Ossory, Ireland yote

**Mei 14-16:** Maridi, Sudani Kusini; Kirinyaga, Kenya; Zaki-Biam & Ijesa Kaskazini-Mashariki, Nijeria na Waikato & Taranaki, New Zealand

# Ufalme Wako Uje

Mei 16-22 2021

## Jumapili 16

Bwana, hebu tuchukue jukumu letu katika kukaribisha ufalme wako leo, kwa kutii ukweli wako, kupenda wengine na kusaidia walio katika hitaji.

## Jumatatu 17

Tunaomba kwamba ufalme wako uje. Tunaomba kwamba kile unachotaka kiweze kufanyika, hapa duniani kama ilivyo mbinguni. *Mathayo 6:10 (ICB)*

## Jumanne 18

Maisha yetu yaonyeshe upendo wako ili tuweze kutunzana na kushiriki mambo mema yote ambayo wewe hutupatia sisi raia wa ufalme wako.

## Jumatano 19

Mungu Muumba, msaidie kila mtu atambue kuwa sisi sote tumeumbwa na wewe na atafute msingi wa mambo yanayofanana kati yetu badala ya kuzingatia tofauti zetu. Hebu kila mtu atangulize kufanya kazi pamoja kwa faida kubwa na atafute njia za kukuza jamii inayojali ambayo inawanufaisha wote.

## Alhamisi 20

Tunapoomba 'Ufalme Wako Uje' sisi sote tunajitolea kushiriki katika kufanywa upya kwa mataifa na mabadiliko ya jamii. *Askofu Mkuu Justin Welby.* Bwana, kwa rehema zako, sikia maombi yetu.

## Ijumaa 21

Bwana, tusaidie kujenga ufalme wako duniani kwa kuishi kwa amani na wengine na kukuza upendo na haki kwa wote. Imarisha imani yetu ili tukuamini wewe kutimiza mahitaji yetu yote hapa duniani tunapotafuta kuishi kwa maadili ya ufalme wako.

## Jumamosi 22

Bwana Mpendwa, tutayarishe ili utakaporudi kwa utukufu utupate tukishughulika juu ya kazi ambayo umeteua kwa kila mmoja wetu kujenga ufalme wako, kazi ambayo tunafanya kupitia neema yako.

### Wimbi la Maombi

**Mei 14-16:** Maridi, Sudani Kusini; Kirinyaga, Kenya; Zaki-Biam & Ijesa Kaskazini-Mashariki, Nijeria na Waikato & Taranaki, New Zealand

**Mei 18-20:** Grahamstown, Afrika Kusini; Masasi, Tanzania; Afikpo, Nijeria; Wiawso, Ghana; Chester, Uingereza na Kaskazini mwa Argentina, Argentina

**Mei 21-23:** Kristo Mfalme, Afrika Kusini; Rwenzori Mashariki, Uganda; Gombe & New Bus, Nijeria na Bunbury, Australia

# Tunda la Roho

## Mei 23-29 2021

**Jumapili 23** Pentekoste

Katika Jumapili hii ya Pentekoste, tujazwe na upendo wako na kushawishika na Roho wako ili tushiriki upendo huo na wote tunaokutana nao katika wiki hii ijayo.

**Jumatatu 24**

Lakini matokeo ya kuongozwa na Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, wema, fadhili, uaminifu, upole na kiasi. Hakuna sheria inayoweza kupinga mambo hayo..
*Wagalatia 5: 22-23*

**Jumanne 25**

Tusaidie, kwa nguvu ya Roho wako, kuongoza njia kwa matendo ya fadhili ambayo yanahitajika ili watu tunaowagusa waje kujua upendo wako.

**Jumatano 26**

Tunapowaona watu wakitenda mambo kwa ubinafsi au tamaa, wakiwatendea wengine mabaya, tusaidie kujizuia ili kuepuka kushiriki katika matendo hayo, na utupe ujasiri wa kubadilisha athari zake.

**Alhamisi 27**

Tukiwa tumejazwa na Roho wako na kuchomwa na shauku ya kuleta upendo kwa wote, Bwana, tupe subira na hekima kujua jinsi na wakati tunavyotakikana kutenda.

**Ijumaa 28**

Fadhili takatifu ni mavazi yangu ya nje, na unyenyekevu uwe mavazi yangu ya ndani'
Bwana tusaidie kuuona ulimwengu kupitia macho yako, kuwa na ujasiri wa kunena dhidi ya udhalimu, na unyenyekevu kutoa msaada usiotambulika.

**Jumamosi 29**

Upendo, furaha, amani, subira, fadhili, wema, uaminifu, upole na kujizuia ni matokeo ya mbegu zilizopandwa kila siku na Roho maishani mwetu. Kila siku, kwa njia ndogo, tuweze kukuza mbegu hizo ndani yetu ili tuonyeshe tunda la Roho linalotokana na hali zote.

### Wimbi la Maombi

**Mei 21-23:,** Christ the King, Afrika Kusini; Rwenzori Mashariki, Uganda; Gombe & New Busa, Nijeria na Bunbury, Australia

**Mei 25-27:** Bor, Sudani Kusini; Mlima Kilimanjaro, Tanzania; Oru & Oleh, Nijeria; Rockhampton, Australia na Agra, India

**Mei 28-30:** Angola; Ankole Kaskazini, Uganda; Okene & Ibadan-Kusini, Nijeria; Aberdeen & Orkney, Scotland na Karnataka Kusini, India

## Jumapili 30

Bwana Yesu, Mfalme wetu wa Amani, tunakumbushwa kupitia Biblia tusiogope bali kukutegemea na kuwa waaminifu katika maombi. Tunakuomba utulize dhoruba za hofu zilizoenea katika ulimwengu wetu wa leo na utuletee amani yako ya kudumu

## Jumatatu 31

Wale ambao ni wapatanishi watapanda mbegu za amani na kuvuna mavuno ya haki.
*Yakobo 3:18*

## JUNI

## Jumanne 1

Baba Mungu, tunaomba kwamba upendo wako wa kudumu utashinda tofauti zote na kwamba utatuma wapatanishi ili kuleta amani kati ya watu walioshikwa katikati ya chuki na mizozo, ambao wanateseka leo.

## Jumatano 2

Baba wa Mbinguni, naomba Serikali za nchi zote duniani zishirikiane kufanya maono yako kwa ajili ya ubinadamu yadhihirike duniani kote. Twaomba wasaidie watu kuishi pamoja kwa maelewano na kupeana msaada kwa kila mmoja.

## Alhamisi 3

Tunamkaribia Mungu wa amani kwa shukrani, kwa vile ametupatanisha kupitia kazi ya msalaba. Tunajitolea kama wapatanishi katika ulimwengu unaolilia amani.

## Ijumaa 4

Bwana wa upendo, tafadhali wabariki watu walio katika nafasi za mamlaka na uwaongoze katika maamuzi yao. Wasaidie kufanya kazi pamoja kuendeleza heshima, haki, na amani.

## Jumamosi 5

Bwana, tusaidie kuishi kwa amani na wengine, natulete upendo na upatanisho katika jamii zetu.

### Wimbi la Maombi

**Mei 28-30:** Angola; Ankole Kaskazini, Uganda; Okene & Ibadan-Kusini, Nijeria; Aberdeen & Orkney, Scotland na Karnataka Kusini, India

**Juni 1-3:** Johannesburg, Afrika Kusini; Kumi, Uganda; Nsukka & Idoani, Nijeria; Derby, Uingereza na Madhya Kerala, India

**Juni 4-6:** Ibba, Sudani Kusini; Maseno Kaskazini, Kenya; Isiala-Ngwa & Ondo, Nijeria; Fredericton, Canada na Amritsar, India

# Kuwakilisha Uumbaji wenye dhamana

6-12 June 2021

## Jumapili 6

Tunaomba tuimbe na kuomba kwa moyo wa shukrani, 'Mshangilieni Mwenyezi-Mungu, enyi nchi zote! Mwabuduni Mwenyezi-Mungu kwa furaha, nendeni kwake mkiimba kwa shangwe!' ...Yeye ndiye aliyetuumba, nasi ni mali yake. *Zaburi 100*

## Jumatatu 7

Basi, Mwenyezi-Mungu akamtwaa huyo mwanamume, akamuweka katika bustani ya Edeni, ailime na kuitunza. *Mwanzo 2:15*

## Jumanne 8

Mungu wa Bustani, tukumbushe kila wakati kuanzisha na kuunda tabia ambazo zitalinda na kuheshimu dunia kwa ajili yetu na kwa wale watakaokuja baada yetu.

## Jumatano 9

Bwana, tusaidie kuelewa umuhimu wa mambo, kwani wakati tunafikiria juu ya jambo fulani, wengine wanaishi na athari zake mbaya, familia zinaondolewa makwao na maisha yanaangamizwa.

## Alhamisi 10

Taka tunazounda zinaonyesha jinsi tunavyoishi maisha yetu. Bwana, ingiza ndani yetu kanuni hii muhimu ya mwongozo katika jukumu letu la kuishi maisha ya uwakili wakati wa maisha yetu duniani.

## Ijumaa 11

Muumba Mungu, umetuumba kwa sura yako ya ajabu kuwa mawakili wa ulimwengu wako. Kwa hivyo tafadhali tusaidie kufanya uchaguzi wenye busara na mwendelevu ili vizazi vijavyo viweze kunufaika katika uumbaji wako badala ya kuteseka kwa vitendo vya ubinafsi ambavyo tumefanya.

## Jumamosi 12

Dunia ni ya Bwana, ni yetu kuifurahia, yetu, kama mawakili wake, kuilima na kuitetea. Bwana mwema utuokoe kutoka kwa uchafuzi wake, matumizi mabaya na uharibifu, ulimwengu bila mwisho. © *Fred Pratt Green, 1903 – 2000*

### Wimbi la Maombi

**Juni 4-6:** Ibba, Sudani Kusini; Maseno Kaskazini, Kenya; Isiala-Ngwa & Ondo, Nijeria; Fredericton, Canada na Amritsar, India

**Juni 8-10:** Yambio, Sudani Kusini; Garissa, Kenya; Mbamili, Nijeria; Hereford, Uingereza; Willochra, Australia na Thailand

**Juni 11-13:** Mahajanga, Madagaska; Mara, Tanzania; West Buganda, Uganda; Kwoi, Nijeria; Newcastle, Australia na Kerala ya Mashariki, India

# Ibada kwa roho na kweli

Juni 13-19 2021

### Jumapili 13

'Baba tunakuabudu, tunaweka maisha yetu mbele zako.' Baba, tunakuletea kila sehemu ya maisha yetu, ili tujazwe na Roho wako Mtakatifu. Tutume ulimwenguni kushiriki zawadi yako na wengine.

### Jumatatu 14

...Wenye kuabudu kwa kweli watamwabudu Baba katika roho na ukweli. Maana Baba anawataka watu wanaomwabudu namna hiyo. *Yohana 4:23*

### Jumanne 15

Bwana Yesu utupe ujasiri wa kutoa maoni yetu ya dhati wakati tunashuhudia dhuluma na ukosefu wa haki katika jamii yetu. Tusaidie kuwa waaminifu kwa ujumbe wako wa upendo kwa wote.

### Jumatano 16

'Roho huishi kutuweka huru, tutembee, tutembee katika nuru.' Natuuthamini uhuru wa kuabudu ambao tunao;  tusiuchukulie kwa urahisi, tukijua kwamba kuna watu wengi ulimwenguni ambao hawafurahii uhuru huo.

### Alhamisi 17

'Ukweli utakuweka huru.' Bwana, tusaidie kuwa waaminifu katika wito wetu -waaminifu kwa wale walio karibu nasi na shuhuda za Injili, kwa maneno na kwa vitendo. Maisha yetu yote na yawe sadaka ya ibada ya kweli.

### Ijumaa 18

'Roho wa utakatifu, hekima na uaminifu, Upepo wa Bwana, ukivuma kwa nguvu na uhuru: nguvu ya kutumikia kwetu na furaha ya kuabudu kwetu - Roho wa Mungu, uniletee utimilifu wako!' Roho Mtakatifu, tuhimize leo tuabudu katika roho na uaminifu.

### Jumamosi 19

Tunaomba tuweze kuwaiga ndugu na dada zetu ulimwenguni kote kwa ibada changamfu yenye furaha, iliyojaa sifa na kuabudu.

### Wimbi la Maombi

**Juni 11-13:** Mahajanga, Madagaska; Mara, Tanzania; West Buganda, Uganda; Kwoi, Nijeria; Newcastle, Australia na Kerala ya Mashariki, India

**Juni 15-17:** Bukavu, DR Kongo; Nyahururu, Kenya; Gboko, Nijeria; Portsmouth, Uingereza na Visiwa vya New Guinea, Papua New Guinea

**Juni 18-20:** Rejaf, Sudani Kusini; Uaskofu wa Jeshi, Kenya; Doko & Owo, Nijeria; Chelmsford, Uingereza na Visiwa vya Jamaika na Cayman

# Matokeo ya kazi yetu

## Kupambana na “njaa ya likizoni” mjini in Down & Dromore, Kusini mwa Ireland

Tangu 2019, Ushirika wa Akina Mama katika Dayosisi ya Down na Dromore, walikuwa wamepanga kushiriki katika “Grub Club” wakati wa likizo ya Pasaka na msimu wa joto wa 2020 kwa kutengeneza kikundi cha kupika na kuwaandalia watoto wanaoathirika na “Njaa ya kwenda likizoni” chakula moto mara mbili kwa wiki. Kanisa la Mount Merrion ndilo lilikuwa limetayarisha mpango huo lakini ilibidi mpango ubadilishwe kwa sababu ya janga la COVID-19. Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama walibadili mpango huo haraka na kutoa msaada wao kwa njia tofauti.

Pia wanasaidia mradi huo kifedha kupitia mchango wao wa “Mums in May”, ambao unatoa misaada ya kusaidia miradi katika jamii kote nchini. Clare Stewart, ambaye ni Mratibu wa Utekelezaji na Uhamasishaji, alisema, ‘Moja ya malengo yetu kama Ushirika wa Akina Mama ni “kusaidia kuleta hali katika jamii inayofaa ili maisha ya familia yawe thabiti, na yasimamie ulinzi wa watoto”, kwa hivyo wakati tuliposikia juu ya mradi wa “Grub Club” ambao Mch Adrian alikuwa akipanga tulipenda sana kuunga mkono mradi kwa kila njia yoyote tunayoweza.”

Kila wiki wakati wa likizo ya shule katika msimu wa joto, kulikuwa na “mini-bootcamp” na zawadi ya chakula cha mchana kwenye uwanja ulio ndani ya mtaa, badala ya mradi uliokuwa umepangwa. Wote walikaribishwa kujiunga, na hadi watu 30 walihudhuria



kila wakati ili kufuata sheria za wakati wa janga la virusi vya Korona zinazohusu utengamano wa kijamii na mikusanyiko ya watu.


Mradi huo pia ulivutia msaada kutoka kwa Active Belfast, ambao walitoa ufadhili kwa maendeleo na utengenezaji wa ishara za kukomesha mazoezi ambazo ziliwekwa kote uwanjani.

Alipoulizwa ni kwa nini kanisa la Mount Merrion lilitaka kutoa huduma hii, Adrian alisema, ‘wazo la “Grub Club”, pamoja na hii “mini-bootcamp” na zawadi ya chakula cha mchana zimeonyesha tu upendo wetu kwa jamii ambayo sisi ni sehemu yake. Wakati wa janga hilo tumetaka kufanya kazi kwa kushirikiana na wengine ili kutoa usaidizi kwa wale walio hatarini zaidi na wale waliotengwa katika eneo hilo. Ni wazi kuwa tuna ukosefu wa fedha na kupitia mpango ambao tunaendesha sasa wa kuchakata sare pamoja na huu mradi wa kila wiki wa kupeana zawadi, tunatumai kushiriki upendo wa Yesu kwa njia ya vitendo. ‘

# Ushirika wa Akina Mama – W



# /anachama Milioni 4 Duniani



# Matokeo ya kazi yetu

## Mabadiliko ya Jamii kupitia kujifunza kilimo, kusoma na kuandika. (CTLA), Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC)

Ushirika wa Akina Mama nchini Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) umeanzisha mradi mpya wa miaka mitatu wa kupunguza unyanyasaji wa kijinsia na umaskini kupitia mafunzo ya kusoma na kuandika na kilimo.

Licha ya utajiri wa maliasili, DRC ni moja ya nchi masikini zaidi duniani. Mwaka wa 2019, zaidi ya robo tatu ya idadi ya watu wake walikadiriwa kuishi chini ya kiwango cha umaskini. Fursa za kiuchumi nchini DRC ni chache sana na zaidi ya 70% ya idadi ya wafanyakazi wameajiriwa katika sekta ya kilimo. Walakini ingawa nchi hiyo ina zaidi ya hekta milioni 80 za ardhi inayoweza kutumiwa kwa kilimo, 10% tu ndio inatumiwa.

Wakati wa MULOA (Ushirika wa Akina Mama unasikiliza, unaangalia na kutenda) na kwa muda wa miaka mingi ambao tumefanya kazi na wanawake walio katika hali ngumu ya maisha, MU DRC iligundua kwamba kutojua kusoma na kuandika ndio kizingiti kikuu kinachokabili idadi kubwa ya jamii katika kuondoa umaskini. Ukosefu wa ujuzi wa msingi wa kusoma na kuhesabu huwazuia kuendesha biashara zao na shughuli za kuongeza mapato, na kunadhoofisha ujasiri wao na uwezo wa kushiriki.

Lengo ni kwamba katika kipindi cha miaka mitatu ya mradi huu, walengwa wataboresha kiwango chao cha kuweza kusoma na kuandika, cha maarifa na ujuzi kuhusu kilimo; wataweza kuanzisha shughuli zao za biashara.



Ili kuona mabadiliko haya, mradi utatoa mpango wa kujifunza kusoma na kuandika, biashara na mafunzo ya ustadi wa kilimo kupitia vikundi vya kijamii vya mafunzo ya kusoma na kuandika, pamoja na vikundi vya uwekaji akiba, mikopo, vyama vya ushirika na vya wakulima. Watu 6,600 katika Dayosisi 12 za Kanisa la Anglikana la Kongo watafaidika.

Mbali na matokeo yake yaliyotarajiwa, mradi unatarajia kuchangia kupunguzwa kwa unyanyasaji wa kijinsia katika kiwango cha kaya na jamii. Pia mradi huu unatarajia kuboresha kiwango cha afya ya msingi, usafi na lishe huku nyenzo na shuhuda zinazotumiwa katika mpango wa kusoma na kuandika zikikuza ufahamu bora na uelewaji wa maswala haya. Vikundi vya kujifunza kusoma na kuandika, vikundi vya kuweka akiba na vyama vya ushirika vya wakulima hutoa nafasi salama ambapo watu wanaweza kushiriki shida na uzoefu wao na kujifunza pamoja bila hofu ya mizozo au kulipiza kisasi.

# Kumkaribisha mkimbizi Juni 20-26 2021

**Jumapili 20** Kumkaribisha mkimbizi
Tunamshukuru Mungu leo kwamba yeye ni Baba yetu kamili wa Mbinguni ambaye anatetea hoja ya yatima na mjane, na anapenda mgeni anayekaa kati yetu, akiwapa chakula na mavazi. *Kumbukumbu la Sheria 10:18*

**Jumatatu 21**
Nilikuwa mgeni nanyi mkanikaribisha; Kweli nawaambieni, kila kitu mlichomtendea mmojawapo wa hawa ndugu zangu wadogo, mlinitendea mimi.' *Mathayo 25: 35, 40*

**Jumanne 22**
Baba Mungu, tunakumbuka mbele yako wote ambao wanapaswa kufanya maamuzi juu ya hali ya wakimbizi. Wawe na huruma, hekima na busara wanaposhughulikia maombi ya wakimbizi.

**Jumatano 23**
Bwana, uliishi kama mkimbizi nchini Misri, ukikimbia hatari na ubabe. Tunaomba tuwe mahali pa kukaribishwa kwa wale wanaotafuta kimbilio kutoka kwa wale ambao watawasababishia madhara, wale wanaowaharibia riziki na maisha yao.

**Alhamisi 24**
Tunawaombea wale waliokata tamaa mpaka wanafanya safari za hatari za kuvuka bahari ili kukimbia hali ya kutokuwa na tumaini, wakitafuta mahali pa usalama. Mahali popote wanapotua tunaomba kwamba wahudumiwe kwa neema, utu na huruma.

**Ijumaa 25**
Tunakumbuka watoto ambao wanakua bila kujua chochote ila kuishi katika hali ya msongamano kwenye kambi za wakimbizi, wale ambao wana njaa na hofu kila wakati.

**Jumamosi 26**
Bwana tunaombea mwitikio wa ulimwengu juu ya mzozo wa wakimbizi ili kuwawezesha wale wanaokimbia hatari kujumuishwa katika jamii ambapo wanaweza kufanya kazi na kutumia ujuzi wao kutunza familia zao.

## Wimbi la Maombi

**Juni 18-20:** Rejaf, Sudani Kusini; Uaskofu wa Jeshi, Kenya; Doko & Owo, Nijeria; Chelmsford, Uingereza na Jamaika & Visiwa vya Cayman

**Juni 22-24:** Rumonge, Burundi; Tabora, Tanzania; Kabba & Bukuru, Nijeria; St Albans, Uingereza na Nagpur, India

**Juni 25-27:** Table Bay, Afrika Kusini; Bonde la Ufa, Tanzania; Evo & Ijebu, Nijeria; Adelaide, Australia na Taejon, Korea Kusini

# Kuendelea Katika Maombi



## Julai-Septemba

**Imeandikwa na Mch Canon Libbie Crossman, Mdhamini wa Ushirika wa Akina Mama wa Kanda C**
**Maandiko matakatifu:** **Msiwe na wasiwasi juu ya kitu chochote, ila kwa kila hali, mwombeni Mungu katika sala juu ya mahitaji yenu, kwa shukrani.** *(Wafilipi 4: 6)*

Nikiwa mtoto mdogo nilimuuliza mama yangu maombi ni nini. Jibu lake limebaki nami, 'Maombi ndio maisha yako yote.' Ingawa nilichukua muda kidogo kuelewa jambo hilo, sasa hivi nikiulizwa swali hili jibu langu ni: 'Maombi ni mazungumzo yetu na Mungu'. Ni jambo la njia mbili na ikiwa ninataka kudumisha uhusiano wangu na Mungu, ninahitaji kudumisha mazungumzo hayo.

Wanachama kutoka Papua New Guinea wanafundishwa tangu utotoni kwamba sala ya kila siku ni sehemu ya maisha yao. Katika hali nyingi sala ya asubuhi kutoka kwa Kitabu cha Maombi ni ibada ya kila siku. Pia kila mwisho wa Ekaristi hakuna anayetoka kanisani mpaka mishumaa itakapozimwa, kwani huu ni wakati wa sala ya kimya.

Msaada mwingine kwa maisha yangu kuhusu maombi ulitokana na mahubiri, wakati bado nilipokuwa mdogo. Mahubiri haya yalitia ndani neno ACTS, (kwa kingereza) kama mfano wa mpangilio katika maombi. Kuabudu, kukiri, shukrani na dua - yaani kuombea matakwa na mahitaji yetu. Nimeutumia mwelekeo huu tangu wakati huo - siwezi kulala bila kuomba na fomula hii - ingawa siku hizi dua kwangu huwa zinapotea ninapouanza usingizi

Kwa hivyo pamoja na maombi ya kawaida na maombi muhimu ya "mshale", ninazungumza na Mungu kila wakati, na ninaweka muda siku nzima wa kumsikiliza Mungu, muda wenye furaha, na natumai hautakoma.

### Hoja za maombi

- Kwa ajili ya kila mkoa kati ya majimbo manne ya eneo la C ili wapone kutokana na athari za COVID-19.
- Kwa wale wanaoomboleza na kujenga maisha yao kwa sababu ya upotezaji wa mapato, vifaa na utulivu.
- Ili familia zaidi zisaidiwe kupitia Mpango wa Ulezi huko Melanesia.



# Mabadiliko

Juni 27-Julai 3 2021

### Jumapili 27
Badilisha maisha yetu, Bwana wa upendo, ili tuweze kuangaza kama taa ulimwenguni, tukionyesha upendo na huruma, tukinyoosha kama mikono na moyo wako duniani.

### Jumatatu 28
Tunabadilishwa tufanane zaidi na huo mfano wake kwa utukufu mwingi zaidi. Hiyo ni kazi yake Roho wa Bwana. *2 Wakorintho 3:18*

### Jumanne 29
Tunakushukuru, Bwana, kwa mwongozo wa Roho wako Mtakatifu katika kutuongoza kwenye maeneo yenye uhitaji, kwa familia zinazojitahidi kukabiliana na shida za maisha, na kwa kutupa ujasiri wako na nguvu ya kuleta mabadiliko kwa wale walio katika shida.

### Jumatano 30
Tunapopambana ili tulete mabadiliko katika jamii na kwa wale wanaoishi  hatarini, katika umaskini, njaa, bila huduma za kimsingi, tusaidie kuwa na ujasiri katika kusimamia wale waliotengwa pembeni mwa ulimwengu.

## JULAI

### Alhamisi 1
Asante, Bwana, kwa maisha yanayobadilishwa kwa nguvu za Roho wako Mtakatifu. Kwa wafungwa wanaopata uhuru kupitia upendo wako. Kwa wale wanaopambana na shida za afya ya akili, waliopewa matumaini ya siku zijazo.

### Ijumaa 2
Bwana, vile ulileta uzuri na mpangilio kutoka gizani na machafuko, tafadhali leta mabadiliko katika ulimwengu wetu ili kuwe na amani na matumaini katika maeneo yenye mizozo na machafuko.

### Jumamosi 3
Baba wa Mbinguni, tunakushukuru kwa kazi ya Ushirika wa Akina Mama, inayoleta mabadiliko, na kwa ajili ya wanachama ambao wanaleta mabadiliko katika jamii zao.

### Wimbi la Maombi

**Juni 25-27:** Table Bay, Afrika Kusini; Bonde la Ufa, Tanzania; Evo & Ijebu, Nijeria; Adelaide, Australia na Taejon, Korea Kusini

**Juni 29-30:** Zambia ya Mashariki, Zambia; Mombasa, Kenya; Gwagwalada & Ekiti-Magharibi, Nijeria; Leicester, Uingereza na Temotu katika Visiwa vya Solomon

**Julai 1-4:** Renk, Sudani Kusini; Cyangugu, Rwanda; Arochukwu / Ohafia & Ile- Oluji, Nijeria; St Andrews, Dunkeld & Dunblane, Scotland na Sittwe, Myanmar

# Haki na rehema

Julai 4-10 2021

## Jumapili 4

Tunakusanyika kama watu wa Mungu leo kumwabudu Bwana na Mfalme wetu mwadilifu; tunaombea ufalme wake hapa duniani. Haki yake iweze kuwaweka huru wafungwa na rehema yake ishinde milele.

## Jumatatu 5

Bwana anasubiri kukuhurumia, na atasimama kukuonyesha huruma. Bwana ni Mungu wa haki; heri wote wanaomngojea. *Isaya 30:18 (CEB)*

## Jumanne 6

Bwana unayetupenda, tusaidie kuchukua jukumu letu katika kutetea haki ili watu wako wastawi na ufalme wako usonge mbele. Na tunapofanya hivi, tuonyeshe rehema yako katika ulimwengu mgumu na wenye kudai.

## Jumatano 7

Tunawaombea leo washirika wetu ulimwenguni kote, ambao wanafanya kazi bila kuchoka na kwa huruma dhidi ya dhuluma za kijamii ambazo zinaathiri maisha ya kifamilia.

## Alhamisi 8

Uniepushe na huruma yako, usiniadhibu kupitia haki yako. *Anselm wa Canterbury, 1033-1109.* Bwana, tunakusifu kwa huruma yako katika Kristo, ambayo inafanya tuokolewe kutokana na matokeo ya haki ya makosa na kasoro zetu.

## Ijumaa 9

Mungu mwenye haki, tunaomba ujasiri wa kupaza sauti tunapoona uvunjwaji wa haki na kusimama na wale wanaotendewa bila haki. Tusaidie kutekeleza amri yako ya kuwapenda majirani zetu kama sisi wenyewe; kuweka ustawi wao mbele ya faraja yetu wenyewe.

## Jumamosi 10

Mungu mwenye Neema, na tuuthamini uhuru tunaoujua kupitia neema yako, na tuwe watu wanaoonyesha huruma katika shughuli zetu zote na wengine.

### Wimbi la Maombi

**Julai 2-4:** Renk, Sudani Kusini; Cyangugu, Rwanda; Arochukwu / Ohafia & Ile- Oluji, Nijeria; St Andrews, Dunkeld & Dunblane, Scotland na Sittwe, Myanmar

**Julai 6-8:** Wad Medani, Sudan; Kondoa, Tanzania; Ikwo & Remo, Nijeria; Montreal, Canada na Visiwa vya Windward, St Lucia, Grenada, St Vincent & The Grenadines

**Julai 9-11:** El Obeid, Sudan; Butere, Kenya; Nnewi, Nijeria; London, Uingereza na Jimbo la USA

# Baraka 

### Jumapili 11
Mungu hutoa baraka zake bila ubaguzi. Wafuasi wa Yesu ni watoto wa Mungu, na wanapaswa kuonyesha sura ya familia hii kwa kutenda mema kwa wote, hata kwa wale wasiostahili kufanyiwa mema. *FF Bruce, msomi wa Biblia, 1910-1990*

### Jumatatu 12
Atukuzwe Mungu na Baba wa Bwana wetu Yesu Kristo! Maana, katika kuungana na Kristo ametubariki kwa kutujalia zawadi zote za kiroho mbinguni.. *Waefeso 1: 3*

### Jumanne 13
Sisi kama wanachama wa Ushirika wa Akina Mama tunatoa shukrani kwa baraka ya kuwa sehemu ya familia ya ulimwengu wote. Tumeunganishwa pamoja katika upendo na huduma. Tunaomba Mungu aendelee kubariki ushirika na umisheni wetu tunapofikia watu kama ifanyavyo mikono yake ulimwenguni kote.

### Jumatano 14
Mungu, tunakushukuru leo kwa baraka za uumbaji wako, ambao kwa uzuri wake huinua roho zetu, na kwa ukuu wake huimarisha imani yetu.

### Alhamisi 15
Baraka za makao, fedha na familia yenye upendo na marafiki ni rahisi sana kuchukulia kawaida. Tunaomba ufahamu zaidi wa baraka ambazo tumepokea na tunaomba utoaji wa Mungu kwa wale ambao wanauhitaji.

### Ijumaa 16
Mungu mkarimu, tunakuletea sifa leo kwa baraka kutoka kwako ambazo tunafurahia katika maisha haya, na ahadi ya baraka ya milele katika ushirika kamili pamoja nawe mbinguni.

### Jumamosi 17
Chukua muda kuomba baraka ya Haruni katika Hesabu 6: 24-26 kwa ajili ya mtu ambaye Mungu amemuweka hususani ndani ya moyo wako leo.

### Wimbi la Maombi

**Julai 9-11:** El Obeid, Sudan; Butere, Kenya; Nnewi, Nijeria; London, Uingereza na Jimbo la USA

**Julai 13-15:** Toliara, Madagaska; Mbale, Uganda; Zaria & Ndokwa, Nijeria; Rochester, Uingereza na Chhattisgarh, India

**Julai 16-18:** Ziwa Malawi, Malawi; Byumba, Rwanda; Jalingo, Nijeria; St Edmundsbury & Ipswich, Uingereza na Lucknow, India

## Imani kwa vitendo

18-24 Julai 2021

### Jumapili 18

Imani kwa vitendo ni upendo - na upendo kwa vitendo ni huduma. *Mama Theresa wa Calcutta*
Bwana leo naniweze kuishi imani yangu kupitia huduma yangu ya upendo kwa wengine.

### Jumatatu 19

Lakini mtu anaweza kusema: "Wewe unayo imani, mimi ninayo matendo!" Haya! Nionyeshe jinsi mtu anavyoweza kuwa na imani bila matendo, nami nitakuonesha imani yangu kwa matendo yangu. *Yakobo 2:18*

### Jumanne 20

Asante, Bwana, kwamba tunapokua katika imani ndivyo tunakua katika kujitolea kwa wale unaotuita kuwatumikia. Tunaomba kwamba tutazidi kuwa tayari kujibu mahitaji yalio karibu nasi kwa kuishi imani yetu kupitia vitendo vya huduma.

### Jumatano 21

Bwana, unatuita, sio ili tujifiche mbali, bali tuangaze kama nuru yako ulimwenguni. Tunaomba leo kwamba nuru ya Kristo ionekane ndani yetu tunapoweka imani yetu kwa vitendo, na kwamba nuru hii itaangaza njia kwa wengine ili waweze kuja kwako.

### Alhamisi 22

Tunapotafuta kuonyesha imani yetu katika vitendo maishani yetu, tuweze kutambua mfano wa Mungu kwenye uso wa jirani yetu na kuwajali kama vile tunamtumikia Kristo.

### Ijumaa 23

Tunashukuru kwa ajili ya wanachama wetu ulimwenguni kote ambao wanashiriki upendo wa Mungu kupitia maisha yao ya vitendo vya uaminifu. Tunawaombea haswa wale wanaotumikia katika mazingira magumu yenye hatari, ili waepushwe na madhara.

### Jumamosi 24

Natuchukue muda leo kutafakari kwa maombi kwa njia mpya ambazo Mungu anatuita kushiriki upendo wake pamoja na wengine tunapoishi kwa imani yetu katika vitendo vyetu.

### Wimbi la Maombi

**Julai 16-18:** Ziwa Malawi, Malawi; Byumba, Rwanda; Jalingo, Nijeria; St Edmundsbury & Ipswich, Uingereza na Lucknow, India

**Julai 20-22:** Gitega, Burundi; Kusini mwa Murang'a na Mbeere, Kenya; Enugu Kaskazini, Nijeria; Polynesia, Tonga na Jaffna katika Dayosisi ya Kanisa la Kusini mwa India

**Julai 23-25:** George, Afrika Kusini; Bungoma, Kenya; Tanganyika ya Magharibi, Tanzania; Itikadi, Nijeria; Sodor & Man katika Kisiwa cha Man na Toronto, Canada

# Afya na uponyaji

Julai 25-31 2021

### Jumapili 25

Mungu wa huruma, tunawaombea wale tunaowajua ambao wanahitaji uponyaji leo, wale wagonjwa katika mwili, akili au roho. Wafunike kwa upendo na upole wako na uwape baraka ya amani yako.

### Jumatatu 26

Mwenyezi-Mungu atamsaidia awapo mgonjwa, atamponya maradhi yake yote
*Zaburi 41: 3*

### Jumanne 27

Baba wa Mbinguni, tunapokiri kwamba uponyaji unatoka kwako, tunawaombea wote wanaohusika katika huduma ya uponyaji; iwe ni wataalamu katika huduma za matibabu, vikundi vya huduma za kanisa, au marafiki na familia ya wale ambao ni wagonjwa.

### Jumatano 28

Ni rahisi sana kupuuza afya yetu ya kiroho tunapokuwa ndani ya shughuli nyingi za kimaisha. Tumwombe Mungu atuongoze leo kwenye maji tulivu, ainue na kuhuisha roho zetu.

### Alhamisi 29

Tunaomba leo kwa ajili ya kazi ya Ushirika wa Akina Mama katika kuhudumia wagonjwa na wanaoteseka, haswa katika maeneo ambayo huduma za afya zinazopatikana ni chache au ghali. Wajumbe wetu na wawe mawakala wa huruma ya Mungu wanapohudumu katika jina lake.

### Ijumaa 30

Tunawaombea wale wote ambao wana wasiwasi juu ya afya zao au za mpendwa wao. Wale wanaofanyiwa vipimo au kusubiri matokeo. Tafadhali tupe huruma na maneno sahihi ya kuleta faraja na matumaini kwa wale ambao wana wasiwasi.

### Jumamosi 31

Bwana, tunakushukuru kwa kuwa wewe ni daktari mkuu ambaye hutufanya kuwa wazima kwa kila njia.

### Wimbi la Maombi

**Julai 23-25:** George, Afrika Kusini; Bungoma, Kenya; Tanganyika ya Magharibi, Tanzania; Itikadi, Nijeria; Sodor & Man katika Kisiwa cha Man na Toronto, Canada

**Julai: 27-29:** Zambia ya Kaskazini, Zambia; Mpwapwa, Tanzania; Gusau & Osun, Nijeria; Sydney, Australia na Rayalaseema, India

**Julai 30 - Agosti 1:** Boga, DR Congo; Manicaland, Zimbabwe; Tanga, Tanzania; Ogoni, Nijeria; Carlisle, Uingereza na Melbourne, Australia

## AGOSTI

### Jumapili 1

Bwana, tusaidie kuchukua nafasi leo ya kukaa pembeni na kupumzika ndani yako. Tunawaombea wale ambao hawana nafasi ya kupumzika siku ya Sabato, ili wapate nafasi ya kuburudika.

### Jumatatu 2

Njooni kwangu, ninyi nyote mliochoka na kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha. Jitieni nira yangu na mjjifunze kwangu, kwa kuwa mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtapata raha kwa nafsi zenu. *Mathayo 11: 28-29*

### Jumanne 3

Tunaomba leo kwamba amani ya Baba wa furaha, amani ya Kristo wa tumaini na amani ya Roho wa neema ziwe pamoja na wale wote walio katika maeneo ya migogoro ambapo utulivu unaonekana kuwa mbali.

### Jumatano 4

Baba wa Mbinguni tunakuletea wazazi wote na walezi wa watoto wadogo ambao huwashughulikia siku nzima, na hata usiku.

### Alhamisi 5

Bwana tunawaombea wale ambao wamelazimishwa kupumzika, hali ya maisha ambayo hawakuipenda. Kwa wazee wadhaifu, wale ambao ni wagonjwa au wenye mapungufu ya kimwili. Wasaidie kujua kwamba wao ni wa thamani kwako na maisha yao yana maana na thamani.

### Ijumaa 6

Mungu mwenye Neema, tunawaombea wote ambao leo wanahisi wamechoka, hawajatulia au wana wasiwasi.

### Jumamosi 7

Mapumziko hutoa utaftaji mzuri wa kuusikia ujumbe wa Mungu tukiwa ndani ya mahangaiko ya maisha. *Shelly Miller, mwandishi.* Bwana zungumza nasi leo tunaposimama kwa muda ili tupumzike na kutafakari. Tuliza akili zetu mbele yako ili tuweze kufunguka kusikia sauti yako na kupumzika katika upendo wako.

### Wimbi la Maombi

**Julai 30-Agosti 1:** Boga, DR Congo; Manicaland, Zimbabwe; Tanga, Tanzania; Ogoni, Nijeria; Carlisle, Uingereza na Melbourne, Australia

**Agosti: 3-5** Juba, Sudani Kusini; Kitale, Kenya; Minna & Lagos, Nijeria; Moray, Ross & Caithness, Scotland na Madurai-Ramnad, India

**Agosti 8:** Malawi ya Kaskazini, Malawi; Eldoret, Kenya; Ngbo & Akure, Nijeria; Kaskazini Magharibi mwa Australia, Australia na Aipo Rongo, PN Guinea

# Maono ya Ushirika wa Akina Mama Agosti 8-14 2021

### Jumapili 8
Bwana unayetupenda, tunapoungana mikono na familia yetu ya Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote, tuwe na umoja katika kusudi letu, tukiongozwa na imani kwa wakati huu, tukiwa na mtazamo kwa ajili ya siku zijazo, ili tuweze kuendelea kutajirisha maisha ya familia kwa ajili ya vizazi vijavyo.

### Jumatatu 9 Siku ya Mary Sumner
Bwana ni mwema. Upendo wake ni wa milele, na uaminifu wake unaendelea kwa kila kizazi. *Zaburi 100: 5*

### Jumanne 10
Naomba kwamba tutaendelea kukua na kujenga juu ya yote tuliyofanikiwa nayo. Na tuendelee kuwa waaminifu kwa malengo yetu huku tukitazamia siku za usoni kwa imani kubwa na matumaini. *Sheran Harper, Rais wa UAM wa Ulimwengu*

### Jumatano 11
Bwana wa jana, leo na hata milele, tusaidie kukabiliana na changamoto za wakati huu wa sasa ili tuweze kufikia maono yetu ya ulimwengu ambapo upendo wako unaonyeshwa kupitia mahusiano ya upendo, heshima na kustawi.

### Alhamisi 12
Bwana mwenye upendo, tunaomba kwamba utuhamasishe kwa maono yako ya siku za usoni ili tuendelee kuwa watu wanaoheshimu na kuabudu jina lako, watu wanaotafuta na kufuata mapenzi yako, wanaofikia ulimwengu kwa upendo wako.

### Ijumaa 13
Mungu mwenye neema, tunakusifu kwa maisha na mahusiano mengi ambayo yamebadilishwa kupitia maono ya washiriki wetu ulimwenguni kote.

### Jumamosi 14
Bwana unayetupenda, tunatoa shukrani kwa mtazamo wa mbali wa mwanzilishi wetu, Mary Sumner. Tusaidie, sisi washiriki wa leo, kuendelea na njia uliyoweka mbele yetu. Tunaposonga mbele kwa shukrani, tunaweka siku zetu za baadaye mikononi mwako.

### Wimbi la Maombi

**Agosti6-8:** Malawi Kaskazini, Malawi; Eldoret, Kenya; Ngbo & Akure, Nijeria; Kaskazini Magharibi mwa Australia, Australia na Aipo Rongo, PN Guinea

**Agosti 10-12:** Niassa, Msumbiji; Masindi Kitara, Uganda; Langtang & Esan, Nijeria; Kaskazini mwa Queensland, Australia na Kolhapur, India

**13-15 Agosti:** Natal, Afrika Kusini; Kajiado, Kenya; Okigwe & Izon Magharibi, Nijeria; Nova Scotia & Prince Edward Island, Canada na Toungoo, Myanmar

## Jumapili 15
Bwana tunashukuru leo kwa ajili ya vijana tunaowajua; kwa hamu yao ya maisha na uwezo wao wa kuzoea mabadiliko. Tunaomba tuwe na unyenyekevu wa kujifunza kupitia mfano wao ili tuweze kuishi maisha makamilifu.

## Jumatatu 16
Hata vijana watafifia na kulegea; naam, wataanguka kwa uchovu. Lakini wote wanaomtumainia Mwenyezi-Mungu, watapata nguvu mpya. *Isaya 40: 30-31 (BHN)*

## Jumanne 17
Tunawaombea leo vijana wote ambao hali ya maisha yao imewasababishia kuelemewa na majukumu yasiyotarajiwa na kukosa furaha ya ujana. Tunaomba wapate fursa ya kufurahia maisha kwa njia inayofaa kulingana na umri wao.

## Jumatano 18
Bwana, utusamehe tunapofanya makosa ya kudhani ujana kuwa kutokea kiakili na kujibu kwa kejeli badala ya uwazi. Tutayarishe milele kufanywa upya na Roho Mtakatifu ili tuweze kuonyesha rehema za Mungu, ambazo ni mpya kila asubuhi.

## Alhamisi 19
Bwana,  tusaidie kuangalia maisha daima kupitia macho ya mtoto, ili tustaajabishwe na ulimwengu uliouumba, ili tuutazame kwa mshangao na sifa.

## Ijumaa 20
Bwana, tusaidie kubaki vijana mioyoni yetu, tukiwa na roho kama ya mtoto ili tutegemee wema wako kuongoza njia zetu, na tusiwe na wasiwasi juu ya kesho.

## Jumamosi 21
Chukua muda leo kufikiria juu ya wale unaowajua ambao wana mtazamo wa ujana maishani mwao, bila kujali umri wao.

### Wimbi la Maombi

**Agosti 13-15:** Natal, Afrika Kusini; Kajiado, Kenya; Okigwe & Izon Magharibi, Nijeria; Nova Scotia & Prince Edward Island, Canada na Toungoo, Myanmar

**Agosti: 17-19** Kasai, DR Congo; Shyira, Rwanda; Ijumu & Egba Magharibi, Nijeria; Liverpool, England na Sambalpur, India

**Agosti 20-22:** Zimbabwe ya Kati, Zimbabwe; Lango, Uganda; Kebbi, Nijeria; Tamale, Ghana; Sheffield, Uingereza na Guadalcanal katika Visiwa vya Solomon

# Kuomba kwa malengo

Agosti 22-28 2021

### Jumapili 22
Bwana, tunakushukuru kwa kutusogelea ili kusikia maombi na dua zetu, kwamba Roho Mtakatifu hutusaidia kuweka mahitaji yetu katika maneno, na kujitetea mbele zako. Maombi yetu na yawe sehemu muhimu katika ujenzi wa ufalme wako duniani.

### Jumatatu 23
Nyinyi mtatuunga mkono kwa kutuombea. Hivyo neema tutakazokuwa tumepata kutokana na maombi ya watu wengi hivyo, ziwe sababu ya watu wengi zaidi kumshukuru Mungu kwa ajili yetu.. *2 Wakorintho 1:11 (NIRV)*

### Jumanne 24
Na tuzidi kuwa na ufahamu juu ya wale wanaohitaji maombi yetu kwa niaba yao, wawe karibu au mbali, na tusichoke kamwe kukuletea mahitaji yao.

### Jumatano 25
Tunaleta maombi yetu kwa Imani, kwa mahitaji yetu au kwa ajili ya wale walio wadhaifu mpaka wameshindwa kuomba. Tunaendelea kutafuta majibu tunayotamani ili tuweze kusonga mbele

### Alhamisi 26
Baba Mungu, tunatamani mabadiliko katika ulimwengu wetu. Tunapoombea mabadiliko katika jamii, maombi yetu na yawe kama mawimbi katika maji, na kufikia maeneo yanayopanuka kila wakati.

### Ijumaa 27
Tunatoa shukrani leo kwa washiriki wetu ambao kwao maombi ni sehemu muhimu zaidi ya kazi zao wanapotumikia jamii zao na kushiriki upendo wa Kristo.

### Jumamosi 28
Kuomba ndio shughuli muhimu zaidi ambayo tunaweza kuwa nayo. Kwani mtu anayeomba hajaridhika kamwe na ulimwengu wa hapa na sasa. Tunajua ya kwamba kuingia katika mazungumzo na Mungu kunawezekana na kwa hivyo tufanye kazi katika kuifanya upya dunia. *Dorothy Friesen, mwandishi na mfanyakazi wa maendeleo ya kanisa*

### Wimbi la Maombi

**Agosti 20-22:** Zimbabwe ya Kati, Zimbabwe; Lango, Uganda; Kebbi, Nijeria; Tamale, Ghana; Sheffield, Uingereza na Guadalcanal, Visiwa vya Solomon

**Agosti 24-26:** Saldanha Bay, Afrika Kusini; Karamoja, Uganda; Udi & Etsako, Nijeria; Wellington, New Zealand na Yangon, Myanmar

**Agosti 27-29:** Matabeleland, Zimbabwe; Mlima Kenya Kati, Kenya; Niger Magharibi, Nijeria; Wangaratta, Australia; Clogher, Ireland yote na Hpa-An, Myanmar

# Misimu mipya

## Agosti 29 - Septemba 4 2021

### Jumapili 29
Bwana unayetupenda, tunakuletea shukrani na sifa zetu kwa uthabiti wako kwa kila msimu wa maisha yetu. Tunatembea kutoka maisha ya zamani hadi yale mapya tukiwa na tumaini na ujasiri, tukijua hutatuacha kamwe.

### Jumatatu 30
Mwenyezi-Mungu atakukinga na baya lolote; atayalinda salama maisha yako. Mwenyezi-Mungu atakulinda katika shughuli zako zote tangu sasa na hata milele.
*Zaburi 121: 7-8*

### Jumanne 31
Baba, tunawaombea watoto na vijana ambao wataingia msimu mpya wa elimu. Na watazamie mbele kwa msisimko wala sio woga, waalimu wao wawe na vifaa vya kuwahamasisha na kuwatunza wanafunzi wao wapya.

### SEPTEMBA
### Jumatano 1
Bwana wa uumbaji, tunakushukuru kwa mabadiliko ya misimu kila mwaka. Tusaidie kuthamini kila msimu, huku tukichukua wakati wa kufurahia sifa za kipekee za kila msimu.

### Alhamisi 2
Mungu mwenye huruma, tunajua kwamba sio misimu yote mipya inayotarajiwa au kukaribishwa. Tunawaombea leo wale wanaolazimishwa kuacha maisha ya kujitegemea au kutoka kwenye nyumba zao wanazozipenda sana kwa sababu ya mabadiliko ya afya au hali ya maisha yao.

### Ijumaa 3
Tunakumbuka katika maombi washiriki wote wanaokusudia msimu mpya wa huduma kwa Ushirika wa Akina Mama, iwe ni jukumu rasmi au mwanzo wa mpango mpya. Roho Mtakatifu na awaongoze na awape uhakika katika njia iliyo mbele yao.

### Jumamosi 4
Bwana, tutayarishe kukubali msimu wowote mpya uliotupangia.

### Wimbi la Maombi

**Agosti 27-29:** Matabeleland, Zimbabwe; Mlima Kenya Kati, Kenya; Niger Magharibi, Nijeria; Wangaratta, Australia; Clogher, All Ireland na Hpa-An, Myanmar

**Agosti 31- Septemba 2:** Harare, Zimbabwe; Machakos, Kenya; Ogori-Magongo & Ekiti, Nijeria; Southwark, Uingereza na Phulbani, India

**Septemba 3-5:** Khartoum, Sudan; Dar es Salaam, Tanzania; Bari & Ilesa, Nijeria; Gloucester, Uingereza na Dugapur, India

# Kufundisha na kujifunza

Septemba 5-11 2021

## Jumapili 5

Fungua mioyo yetu leo ili tujifunze kutoka kwako, ili tujazwe ufahamu wa kina wa Neno lako la thamani na kubarikiwa kwa utajiri wako wa hekima ya kimungu.

## Jumatatu 6

Siku zote kumbuka yale uliyofundishwa. Usikubali kuyaacha. Weka salama yote uliyojifunza. Ni jambo la muhimu zaidi maishani mwako. *Mithali 4:13 (ICB)*

## Jumanne 7

Bwana mwenye Upendo, tunaombea shule zetu zote;  waalimu, wafanyakazi na watoto wanaosoma huko. Ziwe mahali pa kugundua, kujifurahisha na kujifunza; mahali ambapo watoto wanahisi kukubalika na kuwa salama.

## Jumatano 8

Baba wa Mbinguni tafadhali sikia sala zetu kwa wote ambao elimu yao imekomeshwa kwa sababu ya mizozo au hali zingine mbaya za maisha. Tena, kwa ajili ya wanawake na wasichana kote ulimwenguni ambao wananyimwa nafasi za kupata elimu.

## Alhamisi 9

Tunawaombea leo walimu wa watoto ambao wana changamoto fulani za kujifunza.

## Ijumaa 10

Mungu mwenye Neema, utusamehe kwa nyakati ambazo tumepuuza masomo muhimu ya maisha. Tupe roho zinazofundishika ili tuweze kuwa na unyenyekevu wa kujifunza kutoka kwa wengine, hata wale ambao ni wadogo kwetu.

## Jumamosi 11

Bwana Yesu tunakumbuka kwa shukrani watu wote ambao walitufundisha kupitia viwango tofauti vya maisha, waliotusaidia kuchukua hatua ili tuendelee katika safari yetu na wewe. Kwa rehema yako, utatupa pia fursa za kushawishi wengine kwa mema.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 3-5:** Khartoum, Sudan; Dar es Salaam, Tanzania; Bari & Ilesa, Nijeria; Gloucester, Uingereza England na Dugapur, India

**Septemba 7-9:** Pacong, Sudani Kusini; Nyanza Kusini, Kenya; Kutigi & Ijesha Kaskazini, Nijeria; Bristol, Uingereza na Karnataka Kati, India

**Septemba 10-12:** Pretoria, Afrika Kusini; Mbale Kaskazini, Uganda; Oke-Osun, Nijeria; Exeter, Uingereza na Barbados

# Wakati wa mbegu na mavuno Septemba 12-18 2021

## Jumapili 12

Bwana unayetupenda, tunaombea kazi ya Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote, kazi ya kupanda mbegu za matumaini kwa wale ambao wamekata tamaa maishani mwao.

## Jumatatu 13

Na Mungu ampaye mkulima mbegu na mkate kwa chakula, atawapa nyinyi pia mbegu mnazohitaji, na atazifanya ziote, zikue na kuwapa mavuno mengi ya ukarimu wenu.
*2 Wakorintho 9:10*

## Jumanne 14

Bwana, tunakushukuru kwa muujiza wa mavuno; kwa mavuno mengi yanayotokana na mbegu ndogo. Tunawaombea wote wanaohusika katika kuleta mavuno. Hali ya hewa na iwe nzuri na kuwe na idadi ya kutosha ya wafanyakazi.

## Jumatano 15

Bwana wa mavuno, tunakusifu kwa mbegu za maisha ambazo umepanda ndani yetu. Na tutoe mavuno ya haki tunapotafuta kumfuata Kristo na kufanya kazi kwa ukuaji wa ufalme wake duniani.

## Alhamisi 16

Tunawaombea wale kote ulimwenguni ambao wanapata mavuno kidogo kwa sababu ya kutofaulu kwa mazao. Tunaomba kwamba kile wanachokosa kitatolewa na wengine walio na mapato mengi. Wasaidie kutambua mbegu bora za kupanda ili wapate mavuno bora baadaye.

## Ijumaa 17

Bwana mwenye upendo tutume tufanye mapenzi yako katika mashamba ya maisha. Tupe nguvu zako za kuendelea wakati wote wa mabadiliko ya misimu.

## Jumamosi 18

Bwana wa mavuno, tunakushukuru kwa wote ambao wamefanya kazi ardhini na baharini ili kutupatia chakula chetu cha kila siku. Tunakumbuka wale katika nchi zingine ambao wamepanda mbegu na kutunza mazao, ili tupate kufurahia matunda ya kazi zao ndani na nje ya misimu.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 10-12:** Pretoria, Afrika Kusini; Mbale Kaskazini, Uganda; Oke-Osun, Nijeria; Exeter, Uingereza na Barbados

**Septemba 14-16:** Mthatha, Afrika Kusini; Namirembe, Uganda; Pankshin & Sabongidda-Ora, Nijeria; Dublin & Glendalough, Ireland yote na Solomons ya Kati, Visiwa vya Solomon

**Septemba 17-19:** Buye, Burundi; Sebei, Uganda; Abakaliki & Ekiti-Oke, Nijeria; Southwell & Nottingham, Uingereza na Belize

# Amani na usalama

Septemba 19-25 2021

## Jumapili 19

Tunaleta sifa zetu leo kwani sisi kama watoto wa Mungu tunaweza kuwa na uhakika kwamba Kristo ametupatia uzima wa milele na tutaishi naye kwa Amani milele. Asante Mungu kwa tumaini letu la hakika.

## Jumatatu 20

Nawaachieni amani; nawapeni amani yangu. Siwapi nyinyi kama vile ulimwengu ufanyavyo. Msiwe na wasiwasi, wala msifadhaike. *Yohana 14:27*

## Jumanne 21

Bwana, tunaombea amani katika maeneo mengi yanayokabiliwa na shida duniani. Wale walio na mamlaka na ushawishi na wafanye kazi bila kuchoka ili walete amani, ili jamii ziweze kuishi katika sehemu zenye ulinzi na usalama..

## Jumatano 22

Bwana unayetupenda, tunakushukuru sana kwa kila kitu kinachotufanya tujisikie salama- kwa ajili ya nyumba zetu, watu wanaotupenda, na kusudi la maisha.

## Alhamisi 23

Tunashukuru leo kwa wanachama wetu ulimwenguni kote ambao wanafanya kazi na familia na jamii ili kushinda hali zinazosababisha ukosefu wa usalama. Na wawezeshwe kukuza mazingira ambayo husababisha amani ya akili na maisha salama.

## Ijumaa 24

Amani ya kina ya wimbi linalokujia. Amani ya kina ya hewa inayotiririka kwako. Amani ya kina ya dunia tulivu kwako. Amani ya kina ya nyota zinazoangaza kwako. Amani ya kina ya amani isiyo na mwisho kwako. *Baraka ya kiGaelic*

## Jumamosi 25

Chukua muda leo kutafakari kwa maombi juu ya sehemu zozote za maisha yako ambapo unajihisi umekosa usalama na amani. Muombe Mungu aibadilishe hali au akubadilishe wewe mwenyewe, ili uweze kutulia kwa amani yake inayopita kila kitu.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 17-19:** Buye, Burundi; Sebei, Uganda; Abakaliki & Ekiti-Oke, Nijeria; Southwell & Nottingham, Uingereza na Belize

**Septemba 21-23:** Rumbek, Sudani Kusini; Soroti, Uganda; Aba Ngwa Kaskazini & Oyo, Nijeria; Peterborough, Uingereza na Kaskazini Mashariki mwa Caribbean & Aruba

**Septemba 24-26:** Makamba, Burundi; Karamoja Kaskazini, Uganda; Lokoja & Sapele, Nijeria; Truro, Uingereza na Tirunelveli, India

# Furaha ya Maombi



## Oktoba - Desemba

**Imeandikwa na Deborah Chapman, Kiongozi wa Dayosisi ya Ulaya.**
**Maandiko matakatifu Basi, furahini daima katika kuungana na Bwana! Nasema tena: Furahini! . Bwana yu karibu.** *(Wafilipi 4: 4, 5b)*

Ninapenda kufikiria juu ya sala kama kuwa kitu kimoja na moyo wa Mungu - umoja kamili naye na mapenzi yake ya upendo kwa ulimwengu wetu. Wakati moyo wa upendo wa Mungu ulipokuwa mwili ndani ya Yesu (kwa lugha ya Kiebrania "Emmanuel" = Mungu yu pamoja nasi!) Mungu alitukaribia. Na malaika wakasema, "Usiogope." (Luka 1 na 2)

Unabii wa Zefania umetimia katika Yesu. Bwana, Mfalme wa Israeli, yu pamoja nawe; hautaogopa kamwe madhara yoyote... furahini na kushangilia kwa mioyo yenu yote '' (Zefania 3: 15b, 14b). KAMWE ni neno kubwa! Mungu hatuambii kwamba "kamwe hautateseka na maumivu tena ". Hapana - anatuambia kamwe HATUTAOGOPA tena madhara yoyote.

Katika siku tulivu za kuomba na kumsifu Mungu, naachia kila kitu katika mikono yake yenye nguvu na uwezo, nina amani na furaha yenye kina. Na ninajua jinsi Mungu anafurahishwa nami - ninapokea utulivu unaotokana na kujua vile ninapendwa - namsikia akiimba na kufurahi juu yangu ninapoimba kwa kumsifu - sio kwa sababu mimi ni



mkamilifu au mwenye nguvu, lakini kwa sababu katika kutokamilika kwangu na udhaifu wangu, ninamkimbilia - Mungu pamoja nasi! Njoo!

## Hoja za maombi

- Ni jambo gani unaloliogopa? Andika orodha na umletee Mungu kila moja kwa maombi. Unapomsikiliza, futa kila moja na uandike kile Mungu ameweka mahali pake. Furahia uhuru kutoka kwa woga na nguvu inayoleta ili uweze kuishi maisha kikamilifu.
- Rudia ombi hili kutoka kwa Zefania 3:17
    - Ana uwezo wa kuokoa
    - Atafurahi juu yangu sana
    - Atanituliza kwa upendo wake
    - Ataimba furaha yake juu yangu.
- Omba kila siku ujazwe upya kwa Roho Mtakatifu.

## Mashine za kushona kwa wanawake wasiojiweza nchini Rwanda

Wanachama wa Ushirika wa Akina Mama nchini Rwanda wamekuwa wakishughulikia mahitaji ya wenyeji kwa njia ya elimu ya afya, vikundi vya Akiba na Mikopo, amani na upatanisho, msaada kwa wajane, na mafunzo ya ufundi. Mradi mmoja ambao umesaidia wanawake nchini Rwanda kupatia riziki familia zao uliongezewa nguvu na washiriki kutoka Ringmer, Sussex kwenye mkutano wa kahawa ya asubuhi wa Ushirika wa Akina Mama. Washiriki wawili kutoka kikundi cha Ringmer, Sue na Margaret, walitembelea Dayosisi ya Cyangugu, Rwanda mwanzoni mwa mwaka 2019 ambapo waliuona mradi wa ushonaji ambao Berthe, mkewe Askofu wa Cyangugu, alikuwa ameuanzisha.

Berthe aligundua kuwa kulikuwa na akina mama wengi wachanga walioachwa na familia zao. Wanawake hawa walishindwa hata kulisha watoto wao, huku kipato chao kikiwa kidogo sana kwa kupalilia na kulima katika mashamba ya jirani zao. Tena akina mama wengi walikuwa wanalala njaa ili kulisha watoto wao. Aliamua kuanzisha mradi wa UAM kuwafundisha wanawake hawa vijana ushonaji ili kuwapa ujuzi wa kupata pesa zaidi.

Mradi ulikuwa na mashine chache za kushona za kutumiwa na kikundi chote; walihitaji cherehani zaidi ili waweze kusaidia wanawake zaidi. Wanawake hao wangeuza kile walichotengeneza ili wapate pesa zaidi, na hayo yangesaidia



kuwapa heshima ya kuweza kulisha familia zao.

Sue na Margaret walitambua kwamba walihitaji kuongeza vifaa vya kushonea na kuwaelimisha wanawake hao juu ya ushonaji nguo. Mashine za kushona zaligharimu pauni 90 na zilitakiwa kupatikana mahali hapo, ili kusaidia uchumi wa ndani na pia kupunguza gharama za usafirishaji. Wanachama wa UAM wa Ringmer waliamua kufanya mkutano wa kahawa ya asubuhi na kukusanya pesa za kutosha kununua angalau moja ya mashine za kushona wanazotumia. Mkutano ulitangazwa sana na watu wakaanza kuchangia papo hapo. Wengine hata walitoa pesa ya kutosha kununua mashine nzima. Walikusanya pauni 2,000 kwa jumla (au faranga milioni mbili nchini Rwanda), zaidi ya kile kundi lililothubutu kutumainia. Sue na Margaret waliweka faranga milioni mbili mikononi mwa Berthe na Esther, pesa taslimu – zikiwa kwenye mfuko wa karatasi!

# Kuzeeka kwa heshima Septemba 26 - Oktoba 2 2021

## Jumapili 26
Bwana unayetupenda, tunakusifu kwamba unaongozana nasi katika kila msimu; kupitia mabonde na milima

## Jumatatu 27
Njia za watu walio na haki huangaza nuru; kadiri wanavyozidi kuishi, ndivyo wanavyoangaza zaidi. *Mithali 4:18 (Ujumbe)*

## Jumanne 28
Mungu mwenye huruma, tafadhali sikia maombi yetu kwa ajili ya wote wanaoteseka na ugonjwa wa akili wa daimensia. Katika siku ambazo kumbukumbu zao zinabadilika na wakachanganyikiwa, kuwa pamoja nao katika hofu zao.

## Jumatano 29
Bwana Mungu, tunakushukuru kwa vile tunatiwa moyo na Anna na Simeon katika Biblia, ambao walikuhudumia hadi uzeeni wao, wakiendelea kuabudu na kusubiri kwa imani kutimizwa kwa ahadi zako.

## Alhamisi 30
Leo tunawakumbuka wale ambao wanazidi kuhitaji msaada ili kukabiliana na maisha lakini wanaona ni vigumu kukubaliana na hali hiyo.

## OKTOBA
## Ijumaa 1
Bwana tunakushukuru kwa mipango yote ya Ushirika wa Akina Mama ya kutoa msaada na urafiki kufikia wazee. Tunaomba tuweze kusaidia kupunguza upweke, kuimarisha kujiheshimu na kuwa chanzo cha furaha kwa wale walio katika miaka ya uzee.

## Jumamosi 2
Chukua muda leo kutafakari juu ya wazee katika maisha yako ambao wamekuwa wakikutia moyo na kukusaidia kwa miaka mingi.

### Wimbi la Maombi

**Septemba 24-26:** Makamba, Burundi; Karamoja Kaskazini, Uganda; Lokoja & Sapele, Nijeria; Truro, Uingereza na Tirunelveli, India tarehe

**Septemba 28-30:** Katanga, DR Congo; Rwenzori, Uganda; Mbaise & Egba, Nijeria; Meath & Kildare, Ireland Yote na Tiruchirappalli Thanjavur, India

**Oktoba 1-3:** Nzara, Sudan Kusini; Kaskazini Kigezi, Uganda; Kivu, Rwanda; Damataru, Nijeria

# Uanafunzi

3-9 October 2021

## Jumapili 3

Mungu wetu mwenye neema, tunakushukuru kwa kitendawili cha ajabu kwamba ukomavu wa imani unaweza kufikiwa haswa kupitia majibu ya kitoto kwa upendo wako.

## Jumatatu 4

Yesu alisema, 'Ikiwa mnashikilia mafundisho yangu, hakika ninyi ni wanafunzi wangu. Ndipo mtajua ukweli, na ukweli utawaweka huru. ' *Yohana 8: 31-32*

## Jumanne 5

Bwana Mungu, ngao na mlinzi wetu, tunaleta mbele yako washiriki wetu kote ulimwenguni wanapotembea kwenye njia ya uanafunzi, mara nyingi katika mazingira magumu sana. Wahifadhi na uwape amani katika hali zozote wanazokabiliana nazo.

## Jumatano 6

Bwana tunakushukuru kwamba sisi tukiwa wanafunzi wako hatuko peke yetu ila tu sehemu ya familia nzima ya wafuasi. Tusaidie kuhimizana na kusaidiana tunapotafuta mafunzo kutoka kwako na kufuata njia zako pamoja maishani.

## Alhamisi 7

Katika kila hatua ya ukuaji wetu wa Kikristo na katika kila nyanja ya ufuasi wetu wa Kikristo, kiburi ni adui mkubwa na unyenyekevu ni rafiki yetu mkuu. *John Stott, 1921-2011*

## Ijumaa 8

Bwana tufanye tuwe tayari daima, kufuata nyayo zako kwa gharama yoyote kwetu. Tusaidie kuchukua msalaba wetu kila siku kwa furaha, tukitembea kwa imani, popote utakapotuongoza.

## Jumamosi 9

Mwalimu wa Upendo, tusaidie kujifunza na kutiwa moyo na mfano wa wale ambao waliitwa kuwa wanafunzi wako wakati ulikuwa duniani.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 1-3:** Nzara, Sudan Kusini; Kaskazini Kigezi, Uganda; Kivu, Rwanda; Damataru, Nijeria; Auckland, New Zealand na Vanuatu na New Caledonia, Vanuatu

**Oktoba 5-7:** Mbhashe, Afrika Kusini; Kitgum, Uganda; Ukwa & Ilesa Kusini-Magharibi, Nijeria; Tasmania, Australia na Melanesia ya Kati, Visiwa vya Solomon

**Oktoba 8-10:** Ethiopia; Zanzibar, Tanzania; Awgu / Aninri, Nijeria; Freetown, Sierre Leone; Monmouth, Wales na Malaita, Visiwa vya Solomon

## Uhuru na utumwa

## Oktoba 10-16 2021

### Jumapili 10
Kristo Mwokozi wetu, ulikuja kutangaza uhuru kwa wafungwa. Wakati tunapambana kujiondoa kwenye vifungo vya dhambi na ubinafsi, tafadhali fungua ushikilio wao, kupitia upendo wako wa upatanisho, ili tukufuate kwa furaha.

### Jumatatu 11
Amenituma kutangaza kwamba mateka wataachiliwa, kwamba vipofu wataona, kwamba walioonewa watawekwa huru. Luka 4:18 (NLT)

### Jumanne 12
Kuna watu wengi katika jamii ambao wamefungwa na ulevi, unyanyasaji au kiwewe cha mihemko. Wengine kati yao tunawajua vizuri. Tunawaombea leo kwamba Mungu awape njia ya kutoa minyororo yao na kuingia katika maisha ya uhuru.

### Jumatano 13
Ni vigumu kiasi gani kukatazwa kumuabudu Mungu waziwazi. Tunaombea maeneo kote ulimwenguni ambapo watu wananyimwa uhuru huu ambao sisi huchukulia kwa urahisi. Bwana, kwa rehema zako, sikia maombi yetu.

### Alhamisi 14
Asante, Bwana, kwa kazi inayofanywa na washiriki wetu kote ulimwenguni. katika magereza.

### Ijumaa 15
Mungu mwenye haki, tunakuletea sala zetu leo kwa ajili ya wale wote ambao wamefungwa bila hatia au kunyimwa haki zao za msingi za kibinadamu kwa sababu za kisiasa.

### Jumamosi 16
Bwana, tunawaombea waathirika wa uhalifu ambao wapo katika kifungo cha hofu kwa sababu ya mateso waliopitia. Na wapate uhuru kutoka kwa mtego ambao wamekuwa nao maishani mwao, na panapohitajika wapate msaada wa kweli ili wajitoe kutoka hali hizo.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 8-10:** Ethiopia; Zanzibar, Tanzania; Awgu / Aninri, Nijeria; Freetown, Sierre Leone; Monmouth, Wales na Malaita, Visiwa vya Solomon

**Oktoba 12-14:** Ezo, Sudani Kusini; Thika, Kenya; Jos & Akoko, Nigeria; Ulaya na União de Mulheres Episcopais Anglicanas do Brasil (UMEAB), Brazil

**Oktoba 15-17:** Terekeka, Sudan Kusini; Nairobi, Kenya; Maiduguri & Osun Kaskazini, Nijeria; Edinburgh, Scotland na Calcutta, India

# Umasikini na shida

Oktoba 17-23 2021

## Jumapili 17
Mungu mwenye neema, tunakuletea sifa na shukrani zetu leo kwa kutuokoa kutoka katika umaskini wetu wa kiroho na kutupatia utajiri wa wokovu wetu, ambao hutuletea utajiri wa baraka sasa na hata milele.

## Jumatatu 18
Lisha wenye njaa, na uwasaidie wale walio na shida. Ndipo nuru yako itakapong'aa kutoka gizani, na giza lililokuzunguka litakuwa angavu kama adhuhuri. *Isaya 58:10 (NLT)*

## Jumanne 19
Bwana, sikia maombi yetu kwa ajili ya washiriki wetu ulimwenguni kote ambao wanahusika kikamilifu katika changamoto ya kupunguza umaskini. Wawe na rasilimali za kiroho na za vitendo wanazohitaji ili kuendelea kutoa wakiwa katika hali ya ugumu wa maisha.

## Jumatano 20
Tunawaombea leo wale wanaopata shida ya kweli kwa kuwa kipato chao kinawazuia kustahiki msaada wa serikali lakini kidogo sana kuweza kujikimu.

## Alhamisi 21
Umasikini hautengenezwi na Mungu, umeundwa na wewe na mimi wakati hatushiriki kile tulicho nacho. *Mama Teresa wa Calcutta, 1910-1997.* Mungu mkarimu, tusamehe tunapopata visingizio vya kutoshiriki rasilimali zetu na wale walio katika shida.

## Ijumaa 22
Bwana, tunawaombea wote ambao, hata ikiwa wamebarikiwa na utajiri wa mali, wao ni maskini kwa njia zisizoonekana.

## Jumamosi 23
Wakati mwingine tunafahamu umaskini na shida katika nchi nyingine kuliko hapa kwetu. Mungu atupe macho ya kuona kilicho karibu, na mioyo ya kuitikia mahitaji ya majirani zetu.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 15-17:** Terekeka, Sudani Kusini; Nairobi, Kenya; Maiduguri & Osun Kaskazini, Nijeria; Edinburgh, Scotland na Calcutta, India

**Oktoba 19-21:** Viwanja vya Juu Afrika Kusini; Nambale, Kenya; Niger-Delta, Nijeria; Guinea; Blackburn, Uingereza na Bhopal, India

**Oktoba 22-24:** Kimberley na Kuruman, Afrika Kusini; Kitui, Kenya; Kano & Kwara, Nijeria; Armidale, Australia na Myitkyina, Myanmar

# Mfano wa kuvutia

Oktoba 24 -30 2021

## Jumapili 24
Tunaangalia nyuma kwa shukrani kwa wale ambao wamekuwa msukumo katika safari yetu ya kiroho. Tunaomba kwamba sisi pia, tuweze kuhamasisha wengine kujenga maisha yao kwa misingi ya kimungu na yenye thamani.

## Jumatatu 25
Tunakumbuka mbele za Mungu Baba wetu, kazi yako iliyoletwa na imani, bidii yako iliyoongozwa na upendo, na uvumilivu wako uliotokana na tumaini katika Bwana wetu Yesu Kristo. *1 Wathesalonike 1: 3*

## Jumanne 26
Baba wa Mbinguni, tunakusifu kwa msukumo wa Roho Mtakatifu katika maisha yetu; akituonyesha upendo wako, tabia yako na madhumuni yako tunaposoma Neno lako na kutafuta kukua katika imani na kukomaa kiroho.

## Jumatano 27
Bwana wa Upendo, tunatoa shukrani kwa msukumo wa washiriki wetu kote ulimwenguni, ambao hujitolea kwa bidii kutumikia jamii zao kwa jina la Kristo, hata katika ugumu na changamoto katika kazi yao.

## Alhamisi 28
Tunawaombea leo wale wote wasiofurahishwa na kutishwa na kazi zao, zikiwa ni za kulipwa au za nyumbani. Mungu awape ufunuo wa thamani ya kazi yao kwake.

## Ijumaa 29
Ni ngumu kuhamasisha wengine kutimiza yale ambayo wewe mwenyewe haujajaribu kufanya. *(Chanzo hakijulikani)* Bwana, tuhimize ili tufaidi zaidi na yale tunayopata katika maisha yetu; mtazamo wetu maishani uwe msukumo kwa wengine.

## Jumamosi 30
Chukua muda leo ufurahie muziki uupendao, fasihi au sanaa na kumsifu Mungu kwa msukumo wake wa ubunifu ambao huleta mafanikio kama hayo maishani mwetu.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 22-24:** Kimberley na Kuruman, Afrika Kusini; Kitui, Kenya; Kano & Kwara, Nijeria; Armidale, Australia na Myitkyina, Myanmar

**Oktoba 26-28:** Malakal, Sudani Kusini; All Saints Cathedral, Kenya; Kontagora & Osun Kaskazini Mashariki, Nijeria; Glasgow & Galloway, Scotland na Pune, India

**Oktoba 29-31:** Luapula, Zambia; Nakuru, Kenya; Rwenzori Kusini, Uganda; Ibadan- Kaskazini mwa Nijeria; Connor, Ireland yote na Pusan, Korea Kusini

## Watakatifu wa Mungu Oktoba 31 - Novemba 6 2021

### Jumapili 31

Bwana, usiku huu wa manane wa All Hallows, tunaomba kwamba utujaze upya kwa nuru ya uwepo wako, na utukumbushe kwamba mara nyingi tumeona wema wako na neema yako kamilifu.

### NOVEMBA
### Jumatatu 1

Mungu alituokoa na kutufanya watu wake watakatifu. Hiyo haikutokana na chochote tulichofanya sisi wenyewe lakini kwa sababu ya kusudi la Mungu na neema yake.
2 *Timotheo 1: 9 (NCV)*

### Jumanne 2

Bwana, kwa Neno lako unatuita kuwa watakatifu na kujitenga kwa ajili yako. Tunashukuru sana kwamba, ingawa hatuna uwezo wa kufanya hivi kwa nguvu zetu wenyewe,, unatuwezesha kuitikia wito wako kupitia neema yako.

### Jumatano 3

Bwana, tunatoa shukrani kwa ajili ya washiriki wetu kote ulimwenguni ambao wanaangaza taa za utakatifu wako, mara nyingi katika sehemu zenye giza.

### Alhamisi 4

Tunamshukuru Mungu kwa watakatifu wa kila siku katika historia, ambao walijitolea kwa utulivu na matendo ya uaminifu, na kuashiria mwenendo wa utakatifu kizazi hadi kizazi. Tunaomba tuweze kufuata mfano wao katika enzi yetu,  maisha yetu yakiwa yamekusudiwa kutumikia makusudi ya Mungu.

### Ijumaa 5

Bwana Yesu, tusaidie kuishi karibu nawe ili tuweze kuonyesha utakatifu wako katika yote tunayofanya na yote tuliyo.

### Jumamosi  6

Tuchukue muda leo kutafakari kwa maombi juu ya sehemu za maisha yetu ambazo zinaweza kuwa kikwazo kwa kazi ya Mungu ya kuzalisha utakatifu ndani yetu, na tuombe nguvu ya Roho Mtakatifu ituwezeshe kubadilika.

### Wimbi la Maombi

**Oktoba 29-31:** Luapula, Zambia; Nakuru, Kenya; Rwenzori Kusini, Uganda; Ibadan-Kaskazini mwa Nijeria; Connor, Ireland Yote na Pusan, Korea Kusini

**Novemba 2-4:** Lebombo, Msumbiji; Makueni, Kenya; Newala, Tanzania; Niger-Delta Kaskazini, Nijeria; Riverina, Australia na Kaskazini Mashariki mwa India, India

**Novemba 5-7:** Antananarivo, Madagaska; Taita Taveta, Kenya; Ikara & Ife, Nijeria na Argyll & Visiwa, Scotland

### Jumapili 7
Kristo Bwana wetu, tunapochukua mkate na divai leo, tukikumbuka kifo chako kwa shukrani kubwa, tusaidie kufikiria jinsi tunapaswa kuishi kwa kuzingatia dhabihu kama hiyo na zawadi yako ya uzima wa milele.

### Jumatatu 8
Fikiria hayo ninayosema, kwani Bwana atakuwezesha uelewe kila kitu. Mkumbuke Yesu Kristo aliyefufuliwa kutoka kwa wafu, aliyekuwa wa ukoo wa Daudi. *2 Timotheo 2: 7-8*

### Jumanne 9
Mungu wa huruma, leo tunaombea wote walio katika uzee ambao wanapambana na shida ya akili na kupoteza kumbukumbu. Wakiwa katika hali hiyo ya kuchanganyikiwa, waweze bado kujua ukweli wa upendo wako kwao, na wapate kujiskia katika hali ya usalama na amani.

### Jumatano 10
Mwalimu wa Upendo tunaomba msaada wako kwa wote ambao wanajitayarisha kufanya mitihani, ambao wanatakikana wakumbuke na kutafakari juu ya maarifa mengi wanapojitayarisha.

### Alhamisi 11
Bwana, leo tunakumbuka kwa shukrani wote ambao wamejitolea maisha yao ili kulinda uhuru wetu. Tunawaombea wale ambao wanaomboleza kuondokewa mapema na wapendwa wao ambao walitoa dhabihu maisha yao kwa ajili ya wengine.

### Ijumaa 12
Bwana, leo tunafikiria na kuwakumbuka kwa shukrani wale watu tuliowajua zamani, ambao maisha yao yaligusa yetu kwa mema.

### Jumamosi 13
Tuchukue muda leo kukumbuka siku za zamani. Pale kumbukumbu zinatuletea furaha, tuweze kutafakari kwa shukrani. Pale kumbukumbu zimefunikwa kwa uchungu tuweze kujua amani na neema ya Mungu.

### Wimbi la Maombi

**Novemba 5-7:** Antananarivo , Madagaska; Taita Taveta, Kenya; Ikara & Ife,  Nijeria na Argyll & Visiwani, Scotland

**Novemba 9-11:** Kadugli & Nuba Milima, Sudan; Kinkiizi, Uganda; Amichi & Igbomina Magharibi, Nijeria na Ottawa, Canada

**Novemba 12-14:** Ukhahlamba, Afrika Kusini; Maseno Magharibi, Kenya; Mto Oji, Nijeria; Dunkwa-on-Offin, Ghana; Guildford, Uingereza na Coimbatore, India

# Uaminifu

Novemba 14-20 2021

## Jumapili 14

Mwanzoni mwa wiki mpya tunashukuru kwamba chochote kinachotungojea, tunaweza kuutegemea uaminifu wa Mungu daima.

## Jumatatu 15

Basi, jueni kwamba Mwenyezi-Mungu, Mungu wenu, ndiye Mungu; ni Mungu mwaminifu, anayeshika agano lake na huwaonesha fadhili kwa vizazi vingi vya wale wanaoshika amri zake. *Kumbukumbu 7: 9*

## Jumanne 16

Baba wa mbinguni, tunawaombea leo wale wote ambao wanaumia kutokana na kuvunjika kwa uhusiano na kukosewa imani na mtu waliyekuwa wamemwamini. Hata katika maumivu yao, wapate faraja kwa upendo wako thabiti, wa kudumu.

## Jumatano 17

Bwana mwenye upendo, tunakusifu kwa uaminifu wako wa ajabu kwa ajili ya Ushirika wa Akina Mama ulimwenguni kote, kwa miaka mingi.

## Alhamisi 18

Bwana, tunashukuru sana kwamba tunaweza kuweka tumaini letu kwako na kujua kwamba hutatuacha kamwe.

## Ijumaa 19

Bwana, tafadhali utusamehe kwa nyakati ambazo tunayumba katika uaminifu wetu kwako au kwa wengine. Tusaidie kuwa watu wa kuaminika katika nyakati nzuri au mbaya, huku tukiweka ustawi wa wengine mbele ya raha zetu.

## Jumamosi 20

Mungu mwaminifu, tunakusifu kwamba wewe ndiye mwamba ambao tunaweza kutegemea, kwa hali zetu zote. Mwamba imara, ambao unatosha kwetu kusimama juu yake na tukijua tupo kwenye usalama na ulinzi.

### Wimbi la Maombi

**Novemba 12-14:** Ukhahlamba, Afrika Kusini; Maseno Magharibi, Kenya; Mto Oji, Nijeria; Dunkwa-on-Offin, Ghana; Guildford, Uingereza na Coimbatore, India

**Novemba 16-18:** Iraq; Katakwa, Kenya; Kafanchan & Asaba, Nijeria; Lincoln, Uingereza na Trinidad & Tobago

**Novemba 19-21:** Muyinga, Burundi; Ziwa Rukwa, Tanzania; Okrika, Nijeria; St Asaph, Wales

# Kupigania haki ya kijinsia

Novemba 21-27 2021

## Jumapili 21

Mungu wa haki, uliyetuumba sisi sote kwa mfano wako, tunaomba ili watu wote wafuate mfano wako wa kuwatendea wanawake kwa usawa na heshima.

## Jumatatu 22

Ongea kwa ajili ya watu ambao hawawezi kujisemea wenyewe. Linda haki za wote ambao ni wanyonge. *Mithali 31: 8 (GNT)*

## Jumanne 23

Bwana utupendaye, sikia kilio chetu cha haki na uvunje minyororo ya manyanyaso ili watu wote waweze kuishi kwa usalama. Sikia kilio chetu cha kuitaka haki na uvunje minyororo ya ukandamizaji ili watu wote waweze kuishi kwa uhuru, bila kujali jinsia zao.

## Jumatano 24

Tunaomba leo kwa ajili ya kazi ya Ushirika wa Akina Mama duniani kote tunaposhughulikia athari za haki ya kijinsia kwa wanawake na wasichana.

## Alhamisi 25

Tunaombea mahusiano ya kweli na haki kati ya wanawake na wanaume ili pamoja tubadilishe na tushinde vurugu za aina zote, tujifunze kusherehekea utofauti wetu na kutegemeana kwetu. *Baraza la Makanisa Ulimwenguni*

## Ijumaa 26

Bwana Mungu, tunaombea mabadiliko ndani ya serikali na mifumo inayoendeleza uvunjwaji wa haki za kijinsia. Tunaomba mabingwa wanaopigania haki hii wajitokeze, wale ambao wana ushawishi wa kuleta mabadiliko ya kudumu

## Jumamosi 27

Bwana utusamehe kwa vile tumekaa kimya wakati wa uvunjwaji wa haki za kijinsia na tumekataa kupinga vitendo na mitazamo isiyokubalika. Tujaze na azimio jipya la kuwa mabingwa wa haki, kwa jina la Kristo. Amina

### Wimbi la Maombi

**Novemba 19-21:** Muyinga, Burundi; Ziwa Rukwa, Tanzania; Okrika, Nijeria; St Asaph, Wales; Bendigo, Australia na Gujarat, India

**Novemba 23-25:** Kusini mwa Malawi, Malawi; Kaskazini mwa Uganda, Uganda; Lafia & Ilaje, Nijeria na Thoothukudi-Nazareth, India

**Novemba 26-28:** Zululand, Afrika Kusini; Lodwar, Kenya; Isiala Ngwa Kusini, Nijeria; Accra, Ghana; Bangor, Wales na Colombo, Sri Lanka

# Msimu wa Majilio Novemba 29 - Desemba 4 2021

## Jumapili 28
Bwana Mungu, tunapoanza safari yetu ya Majilio ambapo tutakutana na aliyeahidiwa, fungua macho yetu ili tuone maajabu ya kuonekana kwa Kristo; fungua masikio yetu ili tusikie wimbo wa malaika wa wokovu, utufungulie njia ili tulete tumaini maishani mwa wale waliokata tamaa.

## Jumatatu 29
Chipukizi litatokea kutoka shina la Yese, kutoka mizizi yake Tawi litazaa tunda. Roho wa Bwana atakaa juu yake, Roho wa hekima na wa ufahamu, Roho wa shauri na wa uwezo, Roho wa maarifa na wa kumcha Bwana. *Isaya 11: 1-2*

## Jumanne 30
Masia anayetupenda, tusaidie katika msimu huu wa Majilio kutafakari juu ya imani yetu, kuchunguza maisha yetu na safari yetu ya imani hadi sasa.

## DESEMBA
## Jumatano 1
Katika Krismasi hii wakati Kristo atakapokuja, je, atapata moyo mchangamfu? Adhimisha msimu wa Majilio kwa kuwapenda na kuwahudumia wengine kwa upendo na majalio ya Mungu mwenyewe. *Mama Teresa wa Calcutta, 1910-1997*

## Alhamisi 2
Bwana, ufalme wako juu ya maisha yetu ni zawadi ya thamani zaidi kuliko dhahabu. Harufu nzuri ya uwepo wako ni zawadi nzuri kuliko uvumba.

## Ijumaa 3
Mungu mwenye huruma, tunawaombea wote wanaokaribia msimu huu wa Majilio kwa huzuni badala ya furaha. Tunawaombea rehema yako ya upendo wale wanaokabiliwa na Krismasi bila mpendwa wao kwa mara ya kwanza au wale ambao hali zao zimezidi kuwa mbaya katika kipindi cha mwaka huu.

## Jumamosi 4
Tunapojiandaa kukaribisha nuru ya ulimwengu ndani ya mioyo yetu mara nyingine tena, tunajiandaa pia kuwa nuru ulimwenguni, haswa kupitia kazi ya Ushirika wa Akina Mama.

### Wimbi la Maombi

**Novemba 26-28:** Zululand, Afrika Kusini; Lodwar, Kenya; Isiala Ngwa Kusini, Nijeria; Accra, Ghana; Bangor, Wales na Colombo, Sri Lanka

**Novemba 30-Desemba 2:** Mpumalanga, Afrika Kusini; Central Buganda, Uganda; Zonkwa, Nijeria; Bo, Sierra Leone; Newcastle, Uingereza na Barrackpore, India

**Desemba 3-5:** Akot, Sudani Kusini; Kusini Magharibi mwa Tanganyika, Tanzania; Aba & Irele-Ese Odo, Nijeria; Coventry, Uingereza na Cuttack, India

### Jumapili 5
Bwana, tunapojiandaa kusherehekea Krismasi na mihangaiko yake yote, mambo ya kufanya na vitu vya kununua, tusaidie tusisahau kutayarisha mioyo yetu kwa ujio wako kati yetu mara nyingine tena.

### Jumatatu 6
Mtayarishieni Mwenyezi-Mungu njia, nyosheni barabara kuu kwa ajili ya Mungu wetu Kisha utukufu wa Mwenyezi-Mungu utafunuliwa, na watu wote pamoja watauona.
*Isaya 40; 3,5*

### Jumanne 7
Kristo Mwokozi wetu, tafadhali tusaidie kutayarisha njia ya Bwana ili wengine waweze kuuona utukufu wako kupitia matendo yetu ya fadhili na huruma; kwa maneno yetu ya matumaini na upendo. Basi wawe tayari kukuabudu wewe kama Masia wao.

### Jumatano 8
Mungu mwenye huruma, tunawaombea leo wale wote ambao matarajio yao ya msimu huu yanawatia hofu kubwa, kwani ni wakati ambao familia zao zinawashurutisha, na unyanyasaji wa nyumbani unaongezeka.

### Alhamisi 9
Bwana, utusamehe ikiwa miaka imepunguza hisia zetu za matarajio ya kiroho kwa msimu huu.

### Ijumaa 10
Bwana Mungu, tunashangaa tunapotafakari juu ya maandalizi magumu ambayo umefanya kutoka mwanzo wa wakati wa kuja kwa Masia kwa unyenyekevu na kwa kuja kwake tena kwa utukufu.

### Jumamosi 11
Bwana, katikati ya shughuli zetu tusaidie kuweka mbele yetu utakatifu wa wakati huu, tukijiandaa sio tu kwa sherehe za kijuujuu bali kwa kukutana na upendo katika mwili.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 3-5:** Akot, Sudani Kusini; Kusini Magharibi mwa Tanganyika, Tanzania; Aba & Irele-Ese Odo, Nijeria; Coventry, Uingereza na Cuttack, India

**Desemba 7-9:** Namibia; Mlima Kenya Kusini, Kenya; Izon ya Kaskazini & Ijebu Kaskazini, Nijeria na Durham, Uingereza

**Desemba 10-12:** Lusaka, Zambia; Shyogwe, Rwanda; Sokoto & Ikka, Nijeria; Ely, Uingereza na Karimnagar, India

# Muujiza na maajabu

Desemba 12-18 2021

### Jumapili 12

Mungu wa Milele, jaza mioyo yetu kwa mshangao tunapotafakari upya juu ya muujiza wa utukufu wa kuja kwa Kristo duniani kutuletea wokovu; utimilifu wa maneno yako ya unabii, yaliyotamkwa tangu enzi za kale hadi leo.

### Jumatatu 13

Mungu alitaka watu wake kote ulimwenguni waujue utajiri mtukufu wa siri hii-ambayo ni Kristo anayekaa ndani yako, akikupa tumaini la utukufu. *Wakolosai 1:27 (GNT)*

### Jumanne 14

Bwana, ulichagua kujidhihirisha kwa njia isiyotarajiwa; kibanda cha maskini, bakuli la maji na kitambaa na msalaba wa mbao uliokwaruzwa. Tusaidie kuwa kwa hali ya kustaajabu na kushangaa tunapokuabudu.

### Jumatano 15

Muujiza muhimu zaidi unaodaiwa na Wakristo ni Kristo kupata mwili. Wanasema kuwa Mungu alifanyika kuwa Mtu. Kila muujiza mwingine hujitayarisha kwa huu, au huonyesha huu, au ni matokeo ya huu. *CS Lewis, mwanatheolojia, 1898-1962.*

### Alhamisi 16

Baba katika ulimwengu ambao unatafuta ushahidi, ambao unataka maelezo kwa kila tendo na madai, tunaomba kwamba utafungua mioyo na akili ili kuchunguza siri ya ajabu ya mpango wako wa wokovu na kuwa tayari kukusifu kama Bwana wao.

### Ijumaa 17

Tunatazama nyuma kwenye fumbo la jinsi utukufu wa Bwana wa mbingu na dunia ulivyoondolewa katika udhaifu na unyenyekevu wa mtoto mchanga, na kuachwa chini ya utunzaji wa ulimwengu wenye uhasama.

### Jumamosi 18

Chukua muda leo kupumzika katikati ya shughuli nyingi za msimu huu, umuombe Mungu akufungue macho ili upate ufahamu mpya unapotafakari upya ajabu ya Kuzaliwa kwa Yesu.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 10-12:** Lusaka, Zambia; Shyogwe, Rwanda; Sokoto & Ikka, Nijeria; Ely, Uingereza na Karimnagar, India

**Desemba 14-16:** Fianarantsoa, Madagascar; Tanganyika ya Kati, Tanzania; Calabar & Igbomina, Nijeria; Derry & Raphoe, Ireland Yote na Benki na Torres, Vanuatu

**Desemba 17-19:** Lui, Sudani Kusini; Embu, Kenya; Orlu & Awori, Nijeria; Murray, Australia na Medak, India

# Mungu pamoja nasi

Desemba 19-25 2021

## Jumapili 19
Tunaungana leo katika ibada ya kusifu kwamba tunamjia Mungu ambaye hayuko mbali lakini, ambaye, kwa sababu ya Yesu, yuko nasi kabisa katika kila hali ya maisha yetu na katika uhusiano wetu naye.

## Jumatatu 20
Yote haya yalifanyika ili kutimiza yale Bwana aliyosema kupitia nabii: “Bikira atachukua mimba na kuzaa mtoto wa kiume, na watamwita Imanueli” (ambayo inamaanisha “Mungu pamoja nasi”). *Mathayo 1: 22-23*

## Jumanne 21
Bwana, tusamehe kwa wakati tunapotafuta kukuondoa kwenye sehemu ya maisha yetu au hali tunayokabiliana nayo.

## Jumatano 22
Mungu alituambia hasa tumfikirie Yesu kama Imanueli, jina linalomaanisha ‘Mungu pamoja nasi.’ Ni jambo la kushangaza sana kwamba njia kuu ambayo Mungu anataka tufikirie juu ya Yesu ni “kushiriki, kukumbatia maisha kwa Maisha, kitambulisho kamili cha Mungu na kitu anachokipenda.” *Holly Sprink, mwandishi*

## Alhamisi 23
Tunawaombea wote walio katika hali ya upweke na kutengwa, haswa katika msimu huu wa sikukuu. Waijue furaha ya Kristo kwao, inayowapa thamani, ushirika na upendo.

## Ijumaa 24 Mkesha wa Krismasi
Usiku huu, tunasikiliza kwa kustaajabu na imani, kusikia malaika wakitangaza upya habari njema za furaha kuu kwa ulimwengu wote. Tunajitayarisha kuinama na kumwabudu Kristo aliyezaliwa upya.

## Jumamosi 25 Siku ya Krismasi
Wakristo, amkeni, isalimuni asubuhi ya furaha ambayo Mwokozi wa ulimwengu alizaliwa. Inuka kuabudu fumbo la upendo ambalo majeshi ya malaika waliimba kutoka juu.
*John Byrom, 1691-1763*

### Wimbi la Maombi

**Desemba 17-19:** Lui, Sudani Kusini; Embu, Kenya; Orlu & Awori, Nijeria; Murray, Australia na Medak, India

**Desemba 21-23:** Maaskofu wakuu,

# Krismasi

Desemba 26-31 2021

### Jumapili 26
Leo tunapoadhimisha sikukuu ya Mtakatifu Stefano, tunakumbuka mfano wa kujitolea wa Mfalme Wenceslas katika kutunza mtumishi wake; tunawaombea washiriki wetu ulimwenguni kote wanavyojali wanyonge kwa uangalifu na kwa kujitolea

### Jumatatu 27
Nalo Neno likawa mwanadamu, akakaa kwetu. Nasi tumeuona utukufu wake, utukufu wake yeye aliye Mwana wa pekee wa Baba; amejaa neema na ukweli.. *Yohana 1:14*

### Jumanne 28
Tunapokumbuka kwamba hapakuwa na nafasi katika nyumba ya wageni kwa ajili ya mtoto Kristo, tunawaombea wale wasio na makazi, wasiojiweza na waliofukuzwa ulimwenguni kote. Tunatoa shukrani kwa wote wanaotoa mahitaji na makao kwao na tunaombea suluhisho la kudumu lipatikane kwa ajili ya mahitaji yao.

### Jumatano 29
Krismasi ni zawadi ya upendo iliyofungwa katika mwili wa mwanadamu na kufungwa salama kwa ahadi za Mungu zenye nguvu. Maneno hayawezi kueleza, kwani ni jambo la kupokewa moyoni, kuliamini na kulielewa. *Chanzo hakijulikani*

### Alhamisi 30
Tunawaombea wote ambao wameadhimisha Krismasi hii bila kusherehekea Kristo. Mwaka ujao na uwe wakati ambapo watajua zaidi upendo wa Mungu kwao.

### Ijumaa 31
Bwana Mwaminifu, tunasimama katika njia panda kati ya wakati wa zamani na maisha mapya; tunatulia ili kukushukuru kwa baraka zote za mwaka uliopita - na kwa ahadi ya uwepo wako utakaoendelea kwenye mwaka ujao.

### Wimbi la Maombi

**Desemba 24-26:** Wakimbizi, familia zilizohamishwa ndani ya nchi yao na wale wanaoishi katika hali ya hofu

**Desemba 28-30:** Wote wanaohusika na jukumu la kutunza na kusaidia maisha ya familia

# Ombi la Mary Sumner

Ee Bwana, siku ya leo,
nisaidie kugusa maisha mengi
iwezekanavyo kwa ajili yako;
na kila maisha nitakayogusa,
roho wako iyahuishe, iwe ni
kupitia neno nitakalosema,
sala ninayopumua,
au maisha ninayoishi.
Amina.